

UKURASA 20

**Lulu, Wema wazidi kuchefuana**

## Zuio vifungashio vya plastiki lilivyozaa matunda



UKURASA 5


**MAISHA**

Februari 7, 2021 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Jinsi ya kung'arisha dirisha

**Juisi ya Malimao**

Ukurasa 14





**PARACHICHI**

**Tunda linalonogesha, kung'arisha wanawake**

Ukurasa 14

Jumapili Februari 7, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580484



# Bashiru: Viongozi hawa hawatasamehewa CCM

## **Polepole** atumwa kazi maalum bungeni...

*Endelea uk. 2*

UKURASA WA 3

### SERIKALI YAWEKA MASHARTI MAPYA TRA KUFUNGA KIWANDA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Godfrey Mwambe, amesema amekubaliana na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kuamua kufunga kiwanda iwe ni hatua ya mwisho baada ya kutolewa kibali cha Kamishna Mkuu wa...



## USIKOSE MAHOJIANO YA NIPASHE NA RAIS DK. HUSSEIN MWINYI JUMANNE WIKI IJAYO

# Mahakama ya Mafisadi ilivyoipaisha Tanzania

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA, AZAM FC HATUMWI MTOTO UK. 24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Bashiru: Hawa hawatasamehewa CCM

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeanza kufanya tathmini ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka jana, kikisisitiza kuwa hakitamsamehe mtendaji yeyote wa chama atakayebainika kuiba mali, kuhongwa na kuvunja haki ndani ya chama.

Pamoja na hilo, kimewataka wanachama wake kutobweteka na ushindi mkubwa uliopatikana kwenye uchaguzi huo, huku Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, akiagizwa kusikiliza na kuchambua hoja za walio wachache bungeni.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, aliyasema hayo jana jijini hapa katika mdahalo wa uongozi ulioandaliwa na chama hicho ukilenga kuonyesha chama hicho kilikotoka na kinakoelekea, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 44 ya CCM.

Alisema chama hicho kitaendelea kufanya tathmini kwa kila uchaguzi bila kujali ushindi mkubwa uliopatikana na kwa sasa kimeanza kwa ngazi ya chini.

"Tutaendelea kufanya tathmini kwa kila Uchaguzi Mkuu kwa kuwa ndiyo utaratibu wetu wa chama na watakaobainika wamevuruga, iwe watendaji au viongozi, bila kujali ushindi mkubwa tuliopata, lazima hatua kali zitachukuliwa," alisema.

Dk. Bashiru alibainisha kuwa tayari tathmini zimeanza ngazi za chini na zinaendelea kwenye vikao vya kitaifa vitakavyofanyika baada ya kamati kuu kupitisha ratiba na sekretarieti inayosimamia watumishi.

"Kuna maeneo tumechukulia hatua watendaji kwenye mikoa iliyofanya vizuri zaidi kwenye uchaguzi kuliko mahali pengine. Kufanya vizuri siyo utetezi wa kuvunja nidhamu ya chama," alionya.

"Kwa watumishi, tumekubaliana kwenye sekretarieti iliyopita, yeyote atakayebainika kwamba makosa yake yamesababisha kuvunja haki ndani ya chama wakati wa uchaguzi, hata akiwa mtendaji mzuri kiasi gani, hatapewa nafasi ya uongozi ndani ya chama. Yule aliyeiba mali za chama na kuhongwa, hatasamehewa."

Alisema uimara wa chama unatokana na nidhamu na maadili ya chama na viongozi wake na hakuna aliye juu ya msimamo huo.

"Hili halijaanza wakati wa Rais John Magufuli, bali lilianza tangu TANU. Wapo viongozi wa ngazi kubwa walikengeuka na walichukuliwa hatua, kinachofanyika ni kusimamia yaliyoasisiwa. Chama ni wanachama na si watu binafsi," alisema.

**KAZI MAALUM**

Dk. Bashiru alisema kuwa licha ya ushindi mkubwa uliopatikana kwenye uchaguzi uliopita, wanachama wasichukulie ushindi huo kama hakuna mfumo wa vyama vingi na kuwataka kuulinda mfumo huo, ili wasirudi walikotoka.

"Tunaulindaje huo mfumo? Ni kuwasikiliza wale wachache na hoja zao na kuchambua zile hoja zisaidie kujiimarisha zaidi na kuongoza taifa, si wakati kusema hakuna la kujifunza kwa wale tuliowashinda," alionya.

Dk. Bashiru aliwahimiza wale walioshindwa kwenye uchaguzi huo kujenga hoja kwa kuwa kutojenga hoja pia ni kuwaweka katika wakati mgumu kusikiliza mambo ambayo hayana uzito wa kuongezea nguvu kuongoza vizuri.

"Polepole sasa umeingia bungeni, lazima usimamie hili. Hao wabunge wachache waliopo bungeni, wale wa majimbo wawili, wa kutoka Zanzibar na Viti Maalum wana hoja ambazo inabidi chama kisikilize na kuchambua maeneo ambayo tunaweza kutumia kwa kuwa mfumo wa chama unazingatia tupo vyama vingi," aliagiza.

**KIBANO WABUNGE, MADIWANI**

Dk. Bashiru pia alisema demokrasia siyo kushinda uchaguzi peke yake, bali baada ya kushinda uchaguzi, unatimiza ahadi zilizokupa ushindi.

"Tutasimamia walioshinda wajue hiyo siyo dhamana yao kwa kuwa hakuna mgombea binafsi, ni dhamana ya chama na kitawasimamia kuhakikisha yote yanayofanywa, yanahudumia Watanzania wote bila kujali uanachama wao, dini wala kabisa.

"Chama msingi wake ni umoja ambao ni pamoja na kutenda haki. Chama kimejipanga kusimamia wabunge wake, wawakilishi kujenga taifa ambalo litawafanya Watanzania kuwa na maisha bora zaidi. Ukiangalia ilani, ni kazi kubwa na ni mzigo, tumejipanga kuubeba kwa kusimamiana.

"Kuna udhaifu mkubwa kwenye vijiji, vikao havifanyiki ipasavyo, wenyeviti hawatendi haki, hawatoi taarifa za mapato," alisema.

Dk. Bashiru alisema chama kimejipanga kushusha nguvu ya utekelezaji kutoka ngazi ya kitaifa kwenda ngazi za chini hadi vitongoji.

**KUMBUKUMBU 2015**

Akizungumza kuchukua hatua kwa wanachama, mtendaji huyo wa CCM alisema chama hicho ni cha watu na siyo cha malaika.

"Mwaka 2015, matokeo ya uchaguzi hayakuwa mazuri na upande wa Zanzibar hali ilikuwa mbaya. Kwa hiyo, vikao vya chama vikaamua kuteua kamati kwa upande wa Zanzibar iliyoongozwa na Mzee Mangula.

"Ninapenda kutoa taarifa kwamba kazi hiyo ya kamati ndiyo imetupa ushindi mkubwa kuliko wakati wowote kwa mwaka jana kwa upande wa Zanzibar," alisifu.

Alisema kwa upande wa Jamhuri, tathmini ilipofanyika, ilibaini chama kilikuwa kimepoteza nguvu kwa sababu ya makundi na uroho wa vyeo kwa baadhi ya viongozi.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiweka jiwe la msingi katika ujenzi wa Jengo la Hospitali ya Kisasa ya Wilaya ya Kinondoni katika eneo la Mwabwepande, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba na Mkuu wa mkoa huo, Abubakary Kunenge. **PICHA: OMR.**

# Mahakama ya Mafisadi ilivyoipaisha Tanzania

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kimataifa ya Utafiti ya Transparency International (TI), imesema Tanzania imendelea kung'ara katika udhibiti wa vitendo vya rushwa duniani, huku kuanzishwa kwa Mahakama ya Mafisadi kukitajwa kuchangia mafanikio hayo.

Kwa sasa, rekodi za taasisi hiyo zinaonyesha Tanzania inashika nafasi ya 94 kati ya nchi 180 baada ya kupata alama 38 kwa kupambana na rushwa.

Jana, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali John Mbung'o, alisema takwimu hizo za Januari 28, mwaka huu, zinaonyesha Tanzania imepanda kwa alama nane.

Brigedia Jenerali Mbung'o alisema: "Miongozi mwa sababu zilizoipaisha Tanzania katika hatua hiyo ni kutokana na kufunguliwa kwa mahakama maalum inayoshughulikia kesi za ufisadi, makosa ya rushwa na uhujumu uchumi pamoja na watumishi kuwajibika ipasavyo."

Alisema takwimu hizo zinaonyesha namna Tanzania ilivyozipiku nchi 23 ndani ya kipindi cha miaka mitano.

Katika takwimu za taasisi hiyo zilizotolewa mwaka 2015, Tanzania ilipata alama 30 na kushika nafasi ya 117 kati ya nchi 180, zilizofanyiwa utafiti na taasisi hiyo.

"Haya ni mafanikio makubwa kwa kuwa tumepanda alama nane zaidi na kuzipita nchi 23 duniani, siyo kitu cha mchezo, tunastahili pongezi," alisema Brigedia Jenerali Mbung'o.

Alisema kulingana na taarifa hiyo, Tanzania imeshika nafasi ya pili katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Katika orodha hiyo, Tanzania inatanguliwa na Rwanda, wakati kwenye Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yenye wanachama 15, Tanzania imeshika nafasi ya saba.

Sababu nyingine zilizoipaisha Tanzania ni jitihada za serikali kudhibiti na kusimamia maadili ya kwa watumishi wa umma, ikiwemo mikakati ya kupambana na watu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015/16 hadi mwaka 2019/20, TAKUKURU ilifanikiwa kuokoa Sh. bilioni 273.4 zilizokuwa zifujwe kwa njia ya rushwa.

"Ukiacha hilo, wananchi na wadau wamekuwa wakitoa ushirikiano wa kutoa taarifa kwetu, ikiwamo kushiriki katika hatua za uchaguzi na kutoa ushahidi wa kesi zinapofikishwa mahakamani.

"Tunashkuru mchango wa vyombo vya habari kutangaza mafanikio ya serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa. Hii imesaidia Tanzania kufikia nafasi hiyo," alisifu.

Alisema kuwa ili kuhakikisha fedha zinazotolewa na serikali kugharamia miradi ya maendeleo sehemu mbalimbali nchini zinatumika ipasavyo, taasisi hiyo ilifuatilia miradi 3,329 yenye thamani ya Sh. bilioni 12.9.

Katika ufuatiliaji huo, miradi 446 yenye thamani ya Sh. bilioni 87, iligundulika kuwa na kasoro na uchunguzi wake unaendelea.

Alisema pamoja na mafanikio yaliyotajwa na kuchangia Tanzania kushika nafasi hiyo, tatizo la rushwa bado lipo nchini na ili kulikabili, kunahitaji ushiriki wa wananchi pamoja na wadau wote kuisaidia TAKUKURU kuhakikisha vitendo vya rushwa vinatolewa taarifa, ili hatua stahiki za kisheria zichukuliwe.

HABARI KITAIFA

# Serikali yaweka masharti mapya TRA kufunga kiwanda

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Godfrey Mwambe, amesema amekubaliana na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kuamua kufunga kiwanda iwe ni hatua ya mwisho baada ya kutolewa kibali cha Kamishna Mkuu wa mamlaka hiyo.

Amesema wizara yake inakuja na programu maalum inayojulikana kama miliki kiwanda, ambayo itatekelezwa katika kila jimbo la uchaguzi nchini.

Mwambe aliyasema hayo juzi wakati akijibu hoja za wabunge walizozitoa walipokuwa wakichangia bungeni mjadala wa hotuba ya Rais John Magufuli aliyoitoa Novemba mwaka jana wakati akizindua Bunge la 12.

Katika majibu yake, waziri huyo alisema kwa sasa wataalamu wake wanatengeneza programu hiyo ya kumiliki kiwanda ambayo wataipeleka kwenye wilaya na majimbo.

Kutokana na ujio wa programu hiyo, aliwataka wabunge kuwa vinara katika programu hiyo kama Rais Magufuli alivyoelekeza wakati akizindua Bunge hilo.

Kuhusu sekta binafsi, Mwambe alisema sekta hiyo ni changa na hivyo inahitajika kujengwa kwa kupewa fursa ya kufanya biashara.

Vilevile, alimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mpango, kwa kutoa maagizo kwa watendaji wa TRA kuwa kufunga kiwanda iwe hatua ya mwisho baada ya kibali cha Kamishna wa TRA.

"Lakini biashara zote ziko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, ningependa kusisitiza kuwa tuwalee sekta binafsi," alisema Mwambe.

Alisema kuna haja sekta hiyo kueleweshwa juu ya uaminifu kwenye biashara zao na kwamba ni lazima nao wawe na uaminifu ili serikali iwaamini.

Kuhusu mpango mkakati wa serikali (blue print), Mwambe alisema wameanza kutekeleza mpango huo wa kuboresha biashara tangu mwaka juzi, lakini watakuja na mbinu mpya.

Kwa upande wa masoko ya mazao, alisema wanaiboresha Taasisi ya Maendeleo ya Biashara ambayo lengo lake ni kutafuta masomo.

"Tunaenda kupambana kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa nchini zinapata masoko ndani na nje ya nchi," alisema.

Alisisitiza kuwa tayari amekielekeza Chuo cha Biashara (CBE) kutengeneza kozi ambazo zinamjenga mwanafunzi kuwa mfanyabiashara na msimamizi wa biashara.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akipongezwa na wabunge baada ya kuhitimisha mjadala wa Hotuba ya Rais Dk. John Magufuli, aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la 12, Novemba 13, 2020, bungeni jijini Dodoma, juzi. **PICHA: OWM**

# Wabunge wajitosa ujenzi madarasa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WABUNGE wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wametoa mifuko ya saruji 400 kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma ili kusaidia ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Akikabidhi mifuko hiyo juzi, Katibu wa Wabunge hao, Jasson Rweikiza, ambaye ni Mbunge wa Bukoba Vijijini, alisema katika kuadhimisha miaka 44 ya kuzaliwa kwa chama hicho, wabunge wametoa mifuko hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 7.1, ili kusaidia jiji hilo jipya kukabiliana na uhaba wa madarasa.

"Tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani kupitia mkakati wake wa kutoa elimu bure kuanzia shule za msingi hadi sekondari, matokeo ya mkakati huo ni udahili mkubwa wa wanafunzi ambao ni zaidi ya mara tatu kabla ya mkakati huo kuanza kutekelezwa miaka sita iliyopita," alisema.

Aliongeza kuwa kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi, kumewasukuma kulisaidia jiji kukabiliana na uhaba wa miundombinu ya elimu.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Maduka Kessy, alisema mifuko hiyo ya saruji itasaidia kwa kiasi kikubwa katika utatuzi wa uhaba wa madarasa uliopo ambapo kwa mkoa huo, kati ya wanafunzi wa kidato cha kwanza zaidi ya 7,000 waliochaguliwa, 2,000 hawajapangiwa shule kwa kutokana na upungufu wa madarasa.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema mchango huo umeonyesha namna serikali ya CCM inavyojali mahitaji ya wananchi.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Suleiman Serera, alishukuru kwa mchango huo na kusisitiza saruji hiyo itatumika kufyatua matofali ili kufanikisha ujenzi wa madarasa hayo.

# Sheria kulinda mbegu za asili yaandaliwa

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

MABADILIKO makubwa yanatarajiwa katika Sekta ya Kilimo nchini, baada ya serikali kutangaza kutunga sheria mpya ya kulinda mbegu za asili za mazao ya chakula na biashara.

Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Hussein Bashe, amesema sheria hiyo itasaidia mpango wake wa uzalishaji wa mbegu ili kutatua tatizo lililopo nchini.

Kwa sasa, mahitaji ya lazima ya mbegu nchini ni tani 371,000, lakini mbegu zinazozalishwa za kisasa ni tani 76,000. Tani 11,000 ni mbegu ambazo Tanzania inaagiza kutoka nje na mbegu zinazobaki ni mbegu za asili.

Akijibu hoja za wabunge walioigusa Sekta ya Kilimo wakati wa mjadala wa hotuba ya Rais John Magufuli aliyoitoa Novemba mwaka jana alipohutubia Bunge la 12, Bashe alisema Sh. bilioni 179 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa utafiti na uhaulishaji wa mbegu kwa miaka mitano ijayo.

"Tunachokifanya hivi sasa, tunawekeza katika research (utafiti) kwa ajili ya kuendeleza mbegu aina ya OPV na highbred, lakini wakati huo huo kutunza mbegu zetu za asili.

"Sisi kama wizara, Mungu akitujalia tunakuja na sheria maalum ya kulinda traditional seeds (mbegu za asili) ili ziweze kufanyiwa purification (kuchujwa) na ziweze kufanyiwa maendeleo," alisema.

Kwa mujibu wa Bashe, mbegu zinazojadiliwa ni nne ambazo ni za asili, mbegu za OPV, highbred na teknolojia ya GMO (uhandisi jeni).

"Kama nchi, tumesema hatutumii mbegu za GMO (teknolojia ya uhandisi jeni) na hatutaruhusu, na tumeweka utaratibu wa wazi kwamba highbred seeds ambayo tunazungumzia mbegu mbili za kiume na kike zenye sifa mbili tofauti zinazofanyiwa cross breeding (upandikizaji).

"Na hapa msingi wake ni mbegu za asili. Unaweza ukakuta mbegu ya asili A, ina sifa ya uzalishaji mkubwa, lakini haina uwezo wa ku-resist (kuhimili) magonjwa.

"Wataalamu wetu wanafanya kazi ya kuzipandikiza hizi mbegu mbili ili kupata mbegu ambayo ina sifa zote mbili ili kumsaidia mkulima," alifafanua.

**MBEGU ZA MAFUTA**

Kuhusu uzalishaji wa mbegu za mafuta ya alizeti ili kukabiliana na mfumuko wa bei ya mafuta ya kula nchini, Bashe alisema wizara imechukua hatua ya kupambana na tatizo la uhaba wa mafuta hayo.

Bashe alisema hivi sasa, nchi inahitaji uzalishaji wa tani 5,000 za mbegu za highbred na mbegu za opv za alizeti ili kufikia uzalishaji unaotakiwa wa mbegu za mafuta.

Kwenye mazao ya chakula na biashara hasa ngano, Bashe alisema serikali imetia saini hati ya makubaliano (MoU) na wanunuzi wa ngano na uchakataji wa ngano ndani ya nchi, baada ya Wizara ya Kilimo kuweka lengo la kuzalisha tani 150,000 msimu huu.

"Tunatengeneza utaratibu ambao tumekubaliana na sekta binafsi kwamba hatutoagiza ngano kutoka nje kabla ya kununua ngano ya ndani yote.

"Na katika msimu huu unaokuja, tutagawa jumla ya tani 36,000 za mbegu kwa ajili ya kuzalisha ngano katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

"Hapa Dodoma, kule Wilaya ya Bahi, tumefanya pilot study (utafiti) na imeonekana mbegu ina mature (inamea) kwa muda mfupi kuliko wakati wowote na Mkoa wa Rukwa tutagawa hizi mbegu," alisema.

# Ukeketaji watisha, waundiwa mkakati

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

TANZANIA inatajwa kuwa na asilimia 10 ya vitendo vya ukeketaji, ikimaanisha kuwa kwa kila wanawake 100, kumi wamekeketwa.

Kutokana na takwimu hizo, serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji nchini unaotarajiwa kuzinduliwa Machi 15 mwaka huu, kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Watoto Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Sebastian Kitiku.

Aidha, alisema kuna ukeketaji unaofanywa kwa kuvuka mipaka kwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na pembe ya Afrika ili kukwepa mkono wa sheria.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Watoto Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku ya kimataifa ya kupinga ukeketaji mwanamke na mtoto wa kike ambayo hufanyika kila Februari 6.

Alisema mkakati huo wa mwaka 2019 hadi 2022, unalenga kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu kuhusu athari za ukeketaji, kuimarisha mifumo ya kushughulikia keketaji na kuboresha huduma kwa waathirika wa vitendo vya hivyo.

Alisema taarifa ya utafiti wa hali ya watu, afya, na viashiria vya malaria Tanzania(TDHS) ya mwaka 2015/16 inaonyesha kuwa mwanamke mmoja kati ya 10 amekeketwa.

Halikadhalika Kitiku, alitaja mikoa inayoongoza kwa ukeketaji ni Manyara asilimia 58 mwingine ni Dodoma asilimia 47, Arusha asilimia 41, Mara asilimia 32 na Singida asilimia 31.

"Takwimu za kitaifa za ukeketaji ni asilimia 10 na katika mikoa hiyo inaonyesha kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika kutokomeza ukeketaji nchini,"alisema.

Alieleza kuwa sababu zinazotajwa kusababisha wanawake na wasichana kukeketwa ni pamoja na mila na desturi za baadhi ya jamii zinazoamini kwamba ukeketaji unazuia au unatibu magonjwa ya njia ya mkojo.

Mengine alisema ni madai ya kuhifadhi ubikira au usafi wa moyo, inadaiwa unajenga heshima katika familia, fofu ya kutengwa kijamii na wanawake kuamini wasipokeketwa hawajakamilika kuchukua majukumu ya familia waanapoolewa.

Alitaja hatua nyingine ambazo serikali imechukua kuwa ni pamoja na kuandaa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 na kutunga Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 kwa lengo la kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili ukiwamo ukeketaji.

Aidha, alisema serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 ya mwaka 2002, kifungu cha 158(1) (a) ambayo inazuia ukeketaji kwa mtoto wa kike na kutoa adhabu ya faini isiyopungua Sh.500,000 au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja, anayepatikana na hatia.

Kadhalika, alisema kutokana na kuwapo kwa ukeketaji wa kuvuka mipaka, mwaka 2019, nchi za Uganda, Kenya, Somalia na Ethiopia ziliingia makubaliano ya kukabiliana na ukeketaji wa aina hiyo.

"Tanzania tumetekeleza makubaliano hayo kwa kuzijengea uwezo Kamati za Usalama katika wilaya zilizopo vituo vya mipakani vya Sirari (Tarime), Holili (Rombo), Namanga (Longido) na Horohoro (Kilindi) ili kuelewa mbinu zinazotumika kuwasafirisha watoto hao na hatua za kuchukua punde tukio hilo linapotokea,"alisema.

Pia, Wizara kwa kushirikisha halmashauri zilizopo mipakani zimeandaa ujumbe mahsusi wa kuzielimisha jamii kuhusu madhara ya ukeketaji na athari za kusafiri kwa kuvuka mipaka bila vibali.

Akizungumzia kuhusu maadhimisho hayo, mkurugenzi huyo alisema kilele chake kitafanyika kimkoa ambapo wizara itaungana na Mkoa wa Arusha Machi 15, mwaka huu kwenye kuhitimisha.



Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Watoto kutoka Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Sebastian Kitiku (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwenyekiti wa zamani wa CCM afariki dunia

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Erasto Kwilasa, amefariki dunia nchini Kenya, alipokuwa amekwenda kwa ajili ya matibabu.

Wakati wa uchaguzi mkuu wa 2020 Kwilasa alikuwa ni miongoni mwa watiania 60 waliokuwa wanataka kugombea ubunge jimbo la Shinyanga Mjini kupitia CCM. Petrobus Katambi, ndiye mbunge wa jimbo hilo kwa sasa.

Mabala Mlolwa, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho.

"Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha ndugu yetu Erasto Kwilasa kuwa amefariki akiwa nje ya nchi kwa matibabu huko Nairobi tutaendelea kupeana taarifa zaidi," alisema Mlolwa.

Aliongeza kuwa pamoja na siasa Kwilasa alikuwa akijishughulisha na kazi za ukandarasi na kwamba taratibu za kuusafirisha mwili wake kwa ajili ya maziko zinaandaliwa.

Kwilasa alikuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga mwaka 2016 hadi 2017.

**"Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha ndugu yetu Erasto Kwilasa kuwa amefariki akiwa nje ya nchi kwa matibabu huko Nairobi tutaendelea kupeana taarifa zaidi," alisema Mlolwa.**

# Wabunge wa CCM wajenga madarasa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WABUNGE wa CCM wametoa mifuko 400 ya sarauji kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kusaidia ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Akikabidhi mifuko hiyo jana, Katibu wa Wabunge wa CCM , Jasson Rweikiza, ambaye ni mbunge wa Bukoba Vijijini, alisema katika kuadhimisha miaka 44 ya kuzaliwa kwa chama hicho, wametoa mifuko 400 yenye thamani ya Sh. milioni 7.1 kusaidia jiji kukabiliana na uhaba wa madarasa.

"Tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani kupitia mkakati wake wa kutoa elimu bure kuanzia msingi hadi sekondari, matokeo yamekuwa udahili mkubwa wa wanafunzi ambao ni zaidi ya mara tatu kabla ya mkakati huo kuanza kutekelezwa miaka sita iliyopita,"alisema.

Alieleza kuwa kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi kumewasukuma kulisaidia jiji kukabiliana na uhaba wa miundombinu ya elimu.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Maduka Kessy, alisema sementi hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa katika utatuzi wa uhaba wa madarasa uliopo kwani kati ya wanafunzi wa kidato cha kwanza zaidi ya 7,000 waliochaguliwa, 2,000 hawajapangiwa shule kwa sababu ya upungufu wa madarasa.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema mchango huo umeonyesha namna serikali ya CCM inavyojali mahitaji ya wananchi.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Suleiman Serera, aliwashukuru wabunge kwa mchango huo na kusisitiza saruji itatumika kufyatua matofali ili kufanikisha ujenzi wa madarasa hayo kama ilivyokusudiwa.

MAKALA



Waziri waNchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Ummy Mwalimu, akionyesha vifungashio vya plastiki vilivyogeuzwa matumizi na kutumika kama vibebeo vilivyopigwa marufuku.

# Zuio vifungashio vya plastiki lilivyozaa matunda

## • Serikali yawaonya wanaoanza kuvirejesha

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya mwaka mmoja na nusu wa utekelezaji wa maagizo ya serikali ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki kufanikiwa kwa kiasi kikubwa, Tanzania inaanza kushuhudia tena mifuko ya plastiki myeupe ikirudishwa kinyemela sokoni kama vifungashio.

Ni kawaida kukutana na vifungashio hivyo kwa wafanyabiashara wa matunda hasa matikitimaji, mananasi na maembe wakiitumia kuyafunika na kufanga matunda hayo mitaani. Si hivyo tu ndiyo inayotumika madukani kufungasha bidhaa karibu zote kama unga, sukari na mafuta ya kula.

Ukweli ni kwamba kwa kiasi kikubwa katika kipindi chote cha mwaka mmoja na nusu tangu serikali ilipotoa tangazo la kukataza kutumia vifungashio vya plastiki Juni 2019, mafanikio makubwa yalionekana.

Mafanikio haya yanatajwa kuwa ni matokeo ya ushirikiano wa wananchi, taasisi, wazalishaji, wasambazaji na makundi mbalimbali yaliyoshiriki katika kuzingatia maelekezo ya serikali katika kuratibu marufuku ya mifuko ya plastiki.

Mwezi Juni 2019 serikali ilipiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchini kupitia tangazo la Serikali namba 394 lililohusu kuzuia uzalishaji, uingizaji nchini, uuzaji, uhifadhi, usambazaji, matumizi ya mifuko ya plastiki na umiliki mifuko hiyo kwa ajili ya kubebea bidhaa za aina yoyote.

Lengo kuu la marufuku hiyo lilikuwa kulinda mazingira, afya ya binadamu na mifugo dhidi ya athari za matumizi ya mifuko hiyo.

Pamoja na mafanikio haya yaliyopatikana, siku za hivi karibuni , kumejitokeza changamoto ya matumizi ya vifungashio vya plastiki aina ya tubings visivyokuwa na sifa na hivyo kutokukidhi matakwa yaliyowekwa na Shirika la Viwango la Taifa (TBS).

> **kumejitokeza changamoto ya matumizi ya vifungashio vya plastiki aina ya tubings visivyokuwa na sifa na hivyo kutokukidhi matakwa yaliyowekwa na Shirika la Viwango la Taifa (TBS).**

Mapema Januari 8, mwaka huu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Ummy Mwalimu, alitoa tamko kupitia vyombo vya habari la kuonya kuhusu matumizi ya vifungashio vya plastiki kutumika kama vibebeo vya bidhaa na kutoa maelekezo ya serikali.

Kutokana na changamoto hiyo Waziri Ummy alitoa miezi mitatu hadi Aprili 9 mwaka huu kwa wazalishaji na wasambazaji kuhakikisha kwamba vifungashio visivyokidhi viwango vya TBS havipo sokoni.

Ametahadharisha kuwa vifungashio hivi kwa sasa vinazalishwa kwa wingi, kwa ukubwa mbalimbali na vimekuwa vikitumika kama mifuko ya kubebea bidhaa sokoni na kuleta dhana kuwa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku akisema imerudi kivingine kama 'vifungashio'.

Waziri Ummy anafafanua kuwa mifuko hii imeanza kuzagaa kwenye mazingira ya mitaa na vijiji kwa kasi kubwa na hivyo kurudisha nyuma mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi chote cha kupambana na changamoto ya mifuko ya plastiki.

Hata hivyo vifungashio vinavyoruhusiwa katika matumizi mbalimbali kama vile vyakula, sekta ya kilimo, huduma za afya na usafi vinatakiwa kukidhi viwango vilivyowekwa na TBS.

Miongoni mwa viwango hivyo ni pamoja na unene usiopungua microns 30 kwa upande mmoja (single layer) au microns 60 (double layer) pande mbili na viwe na lakiri (seal), ikimaanishwa kuwa kifungashio kinatakiwa kifungashwe na anayefungasha bidhaa yake ili kuuza kabla ya kwenda sokoni. Pamoja na hayo pia vifungashio hivyo vinapaswa kuwa na alama ya mzalishaji au anayepakia bidhaa na viwe na alama ya ubora inayotolewa na TBS.

Kutokana na changamoto hizo Waziri Ummy amewaagiza wasambazaji, wazalishaji na waagizaji wa vifungashio hivi kuacha mara moja kuzalisha, kusambaza, kuuza na kutumia vifungashio hivyo ili kuepuka mkono wa Sheria.

Aidha, kwa mujibu wa waziri tamko hilo limetolewa kwa kuzingatia maombi ya wafanyabiashara wadogo ambao wana shehena ya vifungashio visivyokidhi viwango kuomba kupewa muda wa kuviondosha sokoni, huku akisisitiza kuwa baada ya kipindi hicho, serikali haitatoa tangazo jingine kuhusiana na katazo la matumizi ya vifungashio visivyokuwa na ubora.

Anaongeza kuwa serikali imeanza kuendesha operesheni maalumu kuwabaini wanaozalisha na kusambaza vifungashio visivyokuwa na ubora na kuwachukulia hatua kali kwa mujibu wa sheria hususan wale watakaokaidi.

Pia anawatoa hofu wananchi kuwa hapatakuwapo na uhaba wa vifungashio vinavyokidhi viwango baada ya kipindi hicho cha miezi mitatu kwa kuwa, kwa mujibu wa kanzidata ya TBS kuna wazalishaji wa kutosha wa vifungashio hivyo ili kukidhi mahitaji yaliyopo nchini.

Waziri Ummy anatoa wito kwa wazalishaji na wawekezaji wa ndani kuchangamkia fursa hii kwa kuzalisha vifungashio vyenye kukidhi viwango vilivyowekwa na shirika hilo.

Wazalishaji na wawekezaji wa ndani ambao wangependa kupata ufafanuzi zaidi na mwongozo kuhusu vifungashio vinavyotakiwa wametakiwa kuwasiliana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) pamoja na TBS.

Serikali inasisitiza kuwa ni dhahiri kuwa kila mwananchi analo jukumu kubwa la kulinda na kuyatunza mazingira kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya nchi na kwa faida ya kizazi cha sasa na vingine vijavyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunapaswa kuhoji kabla kupokea chanjo ya corona

CHANJO ya COVID-19 imenza kutumika sehemu mbalimbali duniani wakati takribani watu milioni 104 wameshaambukizwa virusi vya corona huku 2,271,180 (milioni 2.271) wakifariki dunia.

Taarifa zinazotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha ugonjwa huo ni kitisho kipya katika karne hii ya 21.

Wakati chanjo hiyo ikiendelea kutolewa, wapo watu wanaojiuliza maswali mengi kutokana na hofu inayoambatana na kugundulika na kusambazwa kwa kinga hiyo.

Watanzania wamemsikia Rais John Magufuli, akieleza kuwa taifa halitaipokea na kwa sasa ni vyema wakaendelea kujitibu kwa kutumia dawa za asilia na pia kujifukiza, maarufu kupiga nyungu huku tahadhari kama kunawa mikono kwa maji tiririka na kutumia vitakasa mikono ziendelea.

Wapo wanaodhani kuwa ingekuwa vyema kuipokea chanjo hiyo na kuitazama kwa kuchunguza usalama wake, uwezo kitiba na afya ya anayechanjwa ndipo serikali ifanye uamuzi wa kuikataa.

Hali ilivyo duniani leo, takribani watu milioni 100 wameambukizwa na kwa jinsi usambaaji wa maradhi unavyoendelea, ni wazi virusi hivyo vinajiimarisha na kujiunda upya ili kukabiliana na kuishi katika mazingira mapya (mutation) na kwamba upo uwezekano wa kuripotiwa virusi vingi vya aina tofauti katika mataifa mbalimbali kama ambavyo inaelezwa kuwa kuna virusi vipya Afrika Kusini na Ulaya vikipewa jina la N501Y.

Lakini pia zipo taarifa za kuwa na jamii nyingine ya kirusi iliyobadilika na kujiunda upya ambayo ni hatari zaidi inayoitwa 'E484K'ambayo inaelezwa kuwa ina mbinu nyingi za kukwepa mashambulizi yanayofanywa na mfumo wa jeshi la kinga la binadamu na pia kukabiliana na chanjo.

Yote hayo yanazusha maswali kuhusu ubora wa chanjo ya corona na iwapo inaweza kuhimili mikiki ya virusi hivyo vinaelezwa kuwa vinabadilika kila wakati.

Kama taifa, tunapaswa kuangalia jinsi chanjo hiyo ilivyozalishwa kwa kasi na kuanza kusambazwa lakini pia tujiulize mambo mengi kuhusu mabadiliko yanayohusiana na virusi hivyo.

Kwa ujumla, kama Rais alivyosema, hizi ni zama za kuwa makini kwenye masuala yanayohusu chakula, dawa na chanjo zinazotumiwa kwa kuwa matumizi ya sayansi na teknolojia yanaweza kuwa na malengo tofauti hasa ya kusababisha hatari za athari kwa mataifa maskini yasiyo na utaalamu.

Ni jambo lisilofichika kuwa baadhi ya wataalamu wanatumia teknolojia na sayansi kuangalia namna ya kuangamiza baadhi ya jamii duniani kwa kuzalisha mbegu, dawa na hata teknolojia zenye madhara kwa wananchi maskini na hasa wasiokuwa na utambuzi wanaoishi katika mataifa maskini.


Kuna taarifa nyingi kwenye mitandao ya kijamii zinazoeleza kuwa hata mbegu zinazotokana na uchakataji na ubadilishaji wa nasaba (GMO) si salama kwa matumizi ya binadamu.

Mbegu hizo zinaelezwa kuwa zimezalishwa kwa namna ambayo hazibunguliwi na wadudu na hata wakizila wanakufa, mimea hiyo inastawi bila kuhitaji maji mengi, mbolea pamoja na viuatilifu. Yote hayo ni mambo ya kuangalia na kutilia shaka.

Tukirejea kwenye chanjo ya corona, si vyote ving'aavyo ni dhahabu. Kinga ya corona si jambo la kukimbilia kwa sababu, haifahamiki inapotolewa kwa Watanzania na inalenga kupambana na kirusi kipi; cha Covid-19, N501Y au E484K?

Tanzania inapopokea chanjo, inachukua ya kukabiliana na kirusi gani? Yote hayo ni maswali magumu yanayohitaji kujibiwa kabla ya kuigusa dawa hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Katika hili la faru, nampigia saluti JPM

Na Sanula Athanas

**KATIKA** tafsiri ya nguzo kuu za uchumi wa Tanzania, utalii una nafasi kubwa kihistoria. Sekta hiyo sasa inachangia robo ya fedha za kigeni na asilimia 17.5 ya Pato la Taifa.

Kadri mtu anavyozama kuuchambua utalii huo, anaona makundi makuu ya wanyamapori ambao ndiyo vivutio vinavyosafirisha wageni kutoka mbali kuja kuwashuhudia.

Katika makundi hayo, kuna wanyama wakubwa. Moja kwa moja unamgusa mnyama faru. Na hapo ndipo tatizo linapoanzia. Kwanini? Wanyama hao wametoweka kiasi cha kutikisa mwelekeo wa taifa.

Takwimu za Shirika la Uhifadhi Duniani (IUCN), zinabainisha kuwa katika miaka ya 1970, Tanzania ilikadiriwa kuwa na faru 10,000 huku Hifadhi ya Taifa Serengeti pekee ikiwa na wanyama hao wapatao 700. Tayari shirika hilo limeshatangaza kuwa wanyama aina ya faru weusi ambao wako 750 katika Ukanda wa Afrika Mashariki, ni miongoni mwa viumbe vilivyo hatarini kutoweka duniani.

Vilevile, Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF), linabainisha kuwa Tanzania imepoteza takriban asilimia 99 ya faru weusi katika kipindi cha miaka 40 iliyopita.

Sababu ni nini? Mwishoni mwa mwaka jana, Ofisa Mwandamizi wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Philbert Ngoti, alibainisha udhalimu umewakumba wanyamapori hao hata wakatoweka kutoka 10,000 waliokuwapo nchini miaka miaka ya 1970, ndani ya miaka 30 wakabaki 15 tu nchini.

Ngoti ambaye pia Mratibu wa Faru nchini, aliwanyooshea kidole majangili kuwa ni sehemu ya mzizi wa tatizo lililobadili historia ya nchi na hata kuelekea kuwa hasi zaidi.

Alisema Tanzania ni nchi iliyotamba duniani kwa idadi kubwa ya faru, lakini kutokana na baa la ujangili, iligeuka kuwa na hifadhi ya kubahatisha ya wanyama hao, tukio la kiharamia lililozikabili pia nchi nyingi duniani.

Kutokana na hali hiyo, Ngoti alisema serikali ilichukua hatua mbili kuu, ikiwa ni pamoja na ukali uliopitiliza katika ulinzi wa wanyamapori, ambao sasa askari wake wanaowajibika ni jeshi kamili.

Alisema serikali pia iliumiza kichwa kwa njia ya pili inayotokana na faru waliopelekwa ughaibuni Afrika Kusini wakawe mahali salama na rahisi kuzaliana, wakiwa katika hesabu ya wanandugu tisa waliorejeshwa katika hifadhi za nyumbani Novemba 10, 2019.

Ofisa huyo anabainisha kuwa kuchukuliwa kwa hatua hiyo ya nchi kupeana faru, ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kusimamia Viumbe Vilivyo Hatarini Kutoweka (CITES).

Ngoti alisema kuwa katika maisha hayo mapya, faru hao waliotoka ughaibuni na ndugu zao wa nyumbani, jumla yao sasa ni 190, lengo kuu la nchi ni wafike 205 katika miaka mitatu ijayo, yaani kufikia mwaka 2023.

Mtaalamu huyo wa wanyamapori, anafafanua mchakato wa kuzaliana kwamba mimba ya faru inachukua kati ya miezi 15 na 16. Kwa lugha rahisi, ni wastani wa mwaka mmoja na robo.

Binafsi ninampongeza Rais John Magufuli na serikali yake kwa utashi walioonyesha katika kukabiliana na ujangili na kuiepusha nchi kupata fedheha kutokana na kutoweka kwa wanyama hao wakubwa.

Ninaamini kuongezeka kwa idadi ya faru nchini, kumetokana na jitihada zilizofanywa na serikali yake kwa kuanzisha Jeshi la Uhifadhi na kuchukua hatua stahiki dhidi ya majangili na mtandao wao.

Takwimu za TANAPA, zinaonyesha katika miaka mitatu iliyopita, kuna kifo kimoja cha faru nchini ambaye ni Faru Fausta aliyekufa mwishoni mwa mwaka juzi kutokana na ugonjwa.

Hakika, katika hili la kuongezeka kwa idadi ya faru nchini, JPM anastahili pongezi!

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Tutafakari ya JPM na si kuhemka chanjo corona



Nkwazi Mhango, Canada

RAIS John Magufuli, alizua mjadala mkubwa duniani hivi karibuni, pale alipionya wizara ya Afya kutokurupuka kuingiza chanjo za Covid-19.

Wapo waliomshangaa hata kumlaumu kuwa anaweza kuleta madhara makubwa kwa taifa kwa msimamo huu. Pia wapo waliomuunga mkono kwa kuzingatia uzoefu wa bara la Afrika katika mahusiano yake na mataifa ya magharibi pia mfumo kandamizi wa kidunia.

Hii ni jambo la kawaida katika jambo lolote. Wapo watakaokubaliana na hata kutofautiana nalo. Binadamu siyo kama wanyama. Wana uwezo wa kutofautiana, kuelimishana hata kupotoshana.

Kila mmoja ana uhuru wa kutumia maarifa na utashi wake kuliangalia hili.

Hata hivyo, Magufuli siyo pekee mwenye kushuku chanjo na haraka ya kufanya hivyo. Hivi karibuni, kulikuwa na video fupi ya Dk. Nerves Mumba, Mwenyekiti wa chama cha upinzani nchini Zambia, cha the Movement for Multi-Party Democracy (MMD) akitahadharisha serikali ya nchi yake kukurupuka kuagiza chanjo bila ya kujiridhisha kama zinafaa na kuhitajika.

Kuna haja ya kudurusu mantiki ya hoja ya Magufuli kama alivyonukuliwa akisema kuwa "Chanjo hazifai, kama Wazungu wangekuwa na uwezo wa kuleta chanjo, hata chanjo ya Ukimwi ingekuwa imeshaletwa, chanjo ya kifua kikuu ingekuwa kifua ingeshaondoka, hata chanjo ya malaria ingekuwa ishapatikana hata chanjo ya kansa ingekuwa imeshapatikana, lazima Watanzania tuwe waangalifu kwa mambo ya kuletewa letewa." Ukifikiria kwa kina kwa kuangalia maswali aliyouliza na hali alizoziongelea na namna mataifa ya magharibi yalivyoyauzia, kuna mashiko kwenye maswali haya.

Je, kwanini wazungu wamekuwa wepesi kuja na chanjo ya Covid-19 wakati hawakuhamanishwa na majanga aliyotaja Magufuli? Mosi, Covid-19 imewaathiri sana kuliko watu wengine duniani kiasi cha kuhaha.

Mara nyingi, kitu kinachowagusa wazungu, hupewa umuhimu kwa vile chini ya mfumo wa kibaguzi na kikoloni unaendesha dunia, wazungu ndiyo kila kitu.

Pili, wamefanya haraka kuja na chanjo ili kutengeneza fedha. Kwao, kila kitu ni fursa hasa ya kibiashara.

Tatu, pia fursa hii inaweza kutumika kwa kampuni ya madawa si kuuza tu bali kufanya majaribio ya kuboresha na kutumia baadhi ya madawa yake ambayo hayakuwa na soko.

Nne, kutokana na namna Covid-19 inavyoenea haraka, wazungu wasingependa wateketee, wakijiona kama ilivyokuwa kwa waafrika na UKIMWI na Malaria. Kama Malaria ingekuwa inafika Ulaya, bila shaka kinga ingepatikana. Maana ingekuwa inaua 'binadamu' na siyo waswahili.

Baada ya Magufuli kutoa mawazo haya, shirika la Afya duniani lilitoa jibu haraka. Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari kwa njia ya mtandao, mkuu wa WHO kanda ya Afrika Dk. Matshdiso Moeti amesema "Tumeanza kuwasiliana upya na ngazi za juu za uongozi, na tunatoa mchango wetu kama ilivyokua hapo mwanzo, na tunataka kushirikiana na Tanzania, kwa niaba ya watu wa Tanzania, nchi jirani na dunia kwa ujumla. Sehemu ya mawasiliano yetu na Tanzania ni kukumbusha serikali kuwa, hii ni sehemu ya makubaliano ya kanuni za afya za kimataifa ambapo nchi wanachama wamekubali kwa pamoja kuzuia kusambaa kwa magonjwa." Kimsingi, Dk Moeti, hakujibu swali hata moja. Mbona tunapolalamikia matatizo mengine ya kimfumo, mashirika ya Umoja wa Mataifa hayaonekani? Sababu ni rahisi kuwa umaskini siyo sawa na magonjwa hauambukizi wala kuwasumbua matajiri zaidi ya kuwafanya wawe matajiri zaidi. Hivyo, masuala ya kupambana na umaskini pamoja na ukweli kuwa unaua watu wetu wengi, hayawahangaishi wakubwa wa dunia kama yalivyo magonjwa ya kuambukiza tena ambayo yameonyesha kuwaathiri zaidi ya maskini.

Kwanini kuna mantiki?

Ulaya wamekufa sana kuliko Afrika, pamoja na kuwa na huduma bora za kiafya, kuna idadi kubwa ya wazee kuliko Afrika.

Pia ikumbukwe kuwa Ulaya na Amerika ya Kaskazini, hazina vyakula asilia kama ilivyo kwa Afrika. Ulaji unachangia sana kwenye kupambana na magonjwa. Nakumbuka rafiki yangu Adam Ngamange Mkurugenzi Mkuu wa MKIKITA, aliwahi kusema kuwa badala ya kuhangaika na kujenga mahospitali, tutumia fedha na nguvu hii kuelimisha watu wetu juu ya lishe bora jambo ambalo kwa kiwango kikubwa ndilo limeinusuru Afrika.

Mbali na kuwa na vyakula asili na vyenye lishe ambavyo watu wengi wetu hula wakiamini ni vya kimaskini, pia staili za maisha kati ya Ulaya na Afrika ni tofauti.

Ulaya watu wengi wanakufa kwa kula sana tena vyakula visivyo na lishe, huku Afrika watu wakikonda kwa kutokuwa na chakula cha kutosha.

Maisha ya watu wengi Afrika ni zoezi tosha wakati Ulaya watu wanategemea nyenzo kiasi cha kukosa mazoezi. Kutokuwa na magari na vyombo vingine vya moto kunawalazimisha watu wetu wengi kufanya mazoezi bila kutaka wala kujua jambo ambalo kwa Ulaya linakosekana.

Kwanini WHO imekuwa na haraka kuingilia wakati UKIMWI ukifyeka waafrika wala haikuwa na spidi kama hii?

Tumalizie kwa kushauri wahusika kutafakari sana. Kwani janga lipo lakini kwa viwango tofauti kama ilivyo kwa majanga mengine.

Tusiache kujikinga na kuchukua hatua madhubuti lakini bila kukurupuka wala kuhemka yanapotoka mawazo kinzani au fikra mbadala hata kama ni hasi kwa msimamo wa wengine.

Ila hakuna ubishi kuwa kama tutajiridhisha na usalama wa chanjo, tutachanja sawa na wengine. Tanzania siyo kisiwa.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tusiteketeze kila tukamatacho jana



Na Joseph Kulangwa

BODI ya Kusimamia Michezo ya Kubahatisha nchini (GBT), mkoani Singida, imeteketeza mashine 13 za mchezo wa kubahatisha, zilizokamatwa baada ya kubainika ziliingizwa nchini kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za mchezo huo.

Huu ni miongoni mwa michezo ambayo wengine wamekuwa wakiita kamari, na hata wakati mwingine kupigwa marufuku kwa kuwa haramu na wabainikao kuicheza, huchukuliwa hatua kwa kuvunja sheria.

Safi sana, kwamba mashine hizi zimekamatwa baada ya kuingizwa nchini kinyume na taratibu, pengine na kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi ambayo ingelipwa kama hazikupita njia za panya.

Inanikumbusha mwaka fulani maeneo ya Arusha, ambako vifaranga kadhaa vilikamatwa na kuteketezwa moto, baada ya kuingizwa nchini bila taratibu kutoka nchi jirani.

Hatua kama hii pia inaweza kuchukuliwa kwa chakula kinachoingizwa nchini kwa njia hiyo hiyo, au hata bidhaa yoyote inayokiuka sheria, kanuni na taratibu na kukanyaga ardhi ya Tanzania.

Safi kabisa, tunaheshimu taratibu, kanuni na sheria tulizojitungia wenyewe, hakuna wa kulaumu au kulalamikiwa hapo. Unajua kabisa sheria, kanuni na taratibu zipo, wewe kwa makusudi yako unakiuka! Kwa nini visiteketezwe!

Mpaka sasa tunaamini na kujiaminisha, kwamba hatua hiyo ya kuchoma moto bidhaa hizo ndiyo komesha na yenye tija na ni onyo kwa yeyote mwenye nia ya kufanya hivyo. Akiona moto unaviwaka, hatathubutu tena kufanya hivyo.

Naamini adhabu hii inayotolewa kwa bidhaa hizo, zikiwamo mashine na hata wale vifaranga, inavihusu hivyo na bado wamiliki wao nao watakumbana na adhabu stahiki yao, kwa kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Lakini najiuliza, hivi ni kweli kuna tija katika kuteketeza mali hizi au kulikuwa na tija kuteketeza vifaranga wale? Hivi mathalan, wahusika wangechukuliwa hatua kwa ukaidi wao, na mashine hizi wakarudishiwa au la, zikapigwa mnada kingeharibika nini?

Eti, hivi kama mmiliki wa vifaranga wale angechukuliwa hatua na viumbe hao wakaachwa waendelee kukua kwa maslahi yake, au ya wengine hata kama ya watoto yatima, nini kingeharibika?

Hivi mnadhani ni kwa nini JPM amekataa katukatu kusaini wauaji walio magerezani kunyongwa? Anajua kwamba haina tija kuua walioua, kwa sababu ukiwaua waliouawa hawawezi kufufuka.

Lakini mbali na ucha Mungu wake na hofu aliyonayo kwa Maulana wake, anajua akiwanyonga atakuwa amepunguza tu nguvukazi ya Taifa na uzalishaji magerezani utapungua. Kwa nini asiwaache waendelee kulima maisha yao yote na kujilisha, kutulisha na kulisha Taifa!

Tufike mahali tuone ni kipi bora, kwa sababu kupanga ni kuchagua, kama ambavyo tunapokamata magari yaliyofanya makosa ya ama kuingia nchini kipanyapanya au kuingiza magendo, mbona hatuyachomi moto.

Yakikamatwa, tumeshasikia ama yakiuzwa kwa mnada au zikipewa taasisi husuan za usalama, kuyatumia kwa kazi zingine. Kwa nini sasa tuteketeze mashine ambazo zingeweza kutuingizia kipato sisi na Taifa? Kwa nini tuchome moto vifaranga masikini wale, badala ya kuwakuza tuwalie mayai au nyama yao?

Wakati mwingine yatupasa kukaa na kufikiria tu kwamba, angalia, tumekamata pombe kutoka nje ya nchi, imeingia hapa kwa njia ya panya na haiji kumwagilia mimea bali kuuzwa na kunywewa.

Pombe hii tuliyoikamata, kwanza si haramu, tumeipima haina sumu na ikinywewa na Watanzania itawachangamsha, lakini pia itaingiza chochote kwenye fuko la Serikali na chochote hicho kitatumika kutekelezea miradi yetu.

Ona, tuna upungufu wa madarasa na madawati, kutwa kucha tunakimbizana kuhakikisha madarasa yanajengwa na madawati yananunuliwa, ili vitoto visome vimekaa kwenye madawati raha mustarehe, havichomwi jua havinyeshwi mvua wala havijikung'uti mavumbi. Tutajenga na nini kama tutaendelea kuteketeza mashine na vifaranga?

Lakini tukumbuke pia, mashine hizo za michezo ya kubahatisha ni ajira kwa vijana wetu ambao hivi sasa wanasoma wanamaliza shule na vyuo na kurudi kwa baba na mama zao wawatafutie ajira.

Hivyo basi wakijitafutia waachwe watafute, wakikosea wakadakwa wamekiuka waadhibiwe lakini wasiteketezewe mitaji yao, kwa sababu baada ya hapo wataanza tena msako wa mitaji, wakiikosa watajiingiza kwenye uhalifu. Nani atalaumiwa sasa? Alamsiki!

## KONA YA UKWELI

# Polisi Kyela wameshindwa kumtia mbaroni huyu?



Na Thobias Mwanakatwe

Ni Januari 4, 2021 majira ya saa nne asubuhi, ninaiangalia simu yangu ikipigwa kwa namba ambayo siijui. Ninaipokea na kuisikiliza na ninasikia sauti ya mtu mzima anajitambulisha kuwa anaitwa Simon Mwasitu.

Anenieleza shida yake kwamba kuna mfanyabiashara mmoja wa mjini Kyela (anamtaja jina) amemtorosha mtoto wake wa kike ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule ya sekondari ya Itope iliyopo wilayani Kyela.

Anasema tangu amtoroshe mwanafunzi huyo ni siku ya tano na kwamba sasa ameamua kwenda kuripoti katika kituo cha polisi Kyela ili asakwe mfanyabiashara huyo na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Inafika saa sita mchana Mzee Mwasitu ananijulisha kuwa Mfanyabiashara huyo tayari ameshamfunguliwa jalada namba KY4IR/07/2021 katika kituo cha Polisi Kyela na kwamba Jeshi la Polisi lilikuwa limeanza haraka za kumsaka eneo la Matema anakodaiwa "kujichimbia" na binti huyo..

Kama ulivyo utaratibu wa kiuandishi nikampigia simu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei, ambaye ananijulisha kuwa suala hilo wanaendelea kulifuatilia hadi mtuhumiwa huyo akamatwe.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kyela ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wilaya hiyo, Claudia Kitta, alipoulizwa kama anafahamu suala hilo anasema muda huo alikuwa jijini Mbeya kwenye kikao cha Bodi ya Barbara ya Mkoa na kulalamika kwanini mzee Mwasitu anakwenda kulalamikia suala hilo kwenye vyombo vya habari badala ya kwenda ofisini kwake.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo, Simon Mwasitu, kwa uchungu mkali anaeleza kuwa mtoto wake alitoroshwa na mfanyabiashara huyo tangu Disemba 29, 2020 saa 1:30 usiku na kumpeleka kwenye moja ya hoteli za kitalii Matema beach.

Mwasitu anasema ilipofika Disemba 30, 2020 mfanyabiashara huyo alimtuma rafiki yake wa karibu (anamtaja jina) kwenda kuonana na wazazi wa mwanafunzi huyo.

"Rafiki wa mfanyabiashara huyo alipokuja kwangu kuniona alinieleza kuwa ametumwa na mfanyabiashara huyo kwamba tusimtafute mwanafunzi yuko naye na kwamba anaomba amuoe kabisa na yuko tayari kutoa hela atakayohitaji," anasema.

Mwasitu anasema wao kama wazazi walikataa ombi la mfanyabiashara huyo kutaka amuoa mtoto wao kinyume na sheria za nchi, badala yake walimweleza aliyetuma akamwambie kuwa amrejeshe nyumbani mwanafunzi huyo na baada ya kurudi watampima hospitali kuona kama yuko salama na kama atakuwa salama hawatahitaji kuendelea na mambo ya kesi.

Siku tisa baadaye wakati Jeshi la Polisi likiendelea kumsaka mfanyabiashara huyo, mwanafunzi huyo anarejeshwa nyumba kwao kwa kupakizwa kwenye basi kutokea Dar es Salaam na mfanyabiashara huyo ambapo binti huyo anakwenda polisi kutoa maelezo polisi kuthibitisha kwamba alikuwa na mfanyabiashara huyo.

Baada ya kutoa maelezo polisi anapelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela kupimwa ambapo kulingana na maelezo ya baba Mzazi inathibitika kuwa mwanafunzi huyo alibakwa.

Kilichonishtua ni Februari 2, 2021 baada ya baba mzazi wa mwanafunzi huyo aliponipigia simu na kunieleza kuwa mwanafunzi huyo ametoroshwa kwa mara ya pili tena na mfanyabiashara huyo ambapo hadi kufikia siku ya leo amefikisha zaidi ya wiki mbili hajapatikana.

Anasema mtoto wake ametoroshwa pamoja na mwenzake wa kike ambaye naye anasoma katika shule ya sekondari Itope ambapo safari hii mfanyabiashara huyo anadaiwa kutumia njia nyingine kwa kuwatuma vijana wake kuhusika katika utoroshaji wa mwanafunzi hao.

Hata hivyo, nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kuwatia mbaroni vijana hao wanaodaiwa kutumwa na mfanyabiashara huyo kuwatorosha mwanafunzi hao ingawa bado hawajapatikana wala mfanyabiashara.

Kinachowashangaza wananchi wa mji wa Kyela ni kwanini mfanyabiashara huyo hakamatwi anaendelea na matukio haya huku miradi yake aliyoiwekeza Kyela ikiendelea kama kawaida.

Mfano ana ujenzi wa nyumba Kyela unaendelea kama kawaida na muda wote mafundi wake wanachapa kazi na simu zake za mkononi muda wote zinapatikana.

Tukio la kutokamatwa kwa mfanyabiashara huyo ni gumzo kubwa kila kona katika mji wa Kyela ambapo watu wanafika mbali zaidi na kuzungumza mambo mazito dhidi ya Jeshi la Polisi ya kwanini hajakamatwa.

Nafahamu Jeshi letu la polisi liko makini sana katika kutekeleza majukumu yake lakini katika tukio hili kila mwananchi anajiuliza maswali kibao yasiyokuwa na majibu.

Inawezekana Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro hili litakuwa halijakufikia basi kama litakufikia jaribu kuingilia kati ili suala hili ufumbuzi wake upatikane na hivyo maswali kibao yanayoulizwa na wananchi bila majibu yasiendelee.

Hadi naandika uchambuzi huu mfanyabiashara huyo ameshamaliza takribani mwezi hajakamatwa na anaendelea kutanua na mwanafunzi hao huko alikojichimbia.

***Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com***

***MUNGU IBARIKI TANZANIA***

## DARASA LA NDOA

# Utatuzi na utawala wa migogoro ya ndoa



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka

UTATUZI na utawala wa migogoro ni somo muhimu sana hasa katika nyakati hizi za sasa ambapo tunashuhudia migogoro mingi na kuvunjika kwa ndoa nyingi katika jamii.

Inawezekana wanandoa wanapendana, lakini wakajibizana na kugombana mara kwa mara. Jambo dogo likakuzwa na kuwa tatizo kubwa. Ugomvi unaweza kutokea kwa sababu ya tofauti za uelewa na mitazamo katika jambo husika.

Hii ni hali ya kawaida ambayo hutokea katika maisha ya binadamu. Ni sehemu ya joto la uhusiano. Hii inatokana na ukweli kuwa dunia inatawaliwa na mwanadamu, ambaye ni kiumbe wa pekee na wa ajabu.

Migogoro ya wanandoa wengi, kwa sehemu kubwa, hutokana na masuala yanayohusu majukumu ya kifamilia, watoto, fedha, tabia, mienendo, mawasiliano, ndugu, marafiki, jamaa, na tendo la ndoa.

Inawezekana wanandoa wengine wamejitahidi kutatua migogoro yao, lakini pasipo mafanikio. Kadiri siku zinavyokwenda, migogoro imeota mizizi na kuchukua sura mpya kiasi cha wanandoa kufikiria kutengana au kuachana. Hali hii imenisukuma kuandika mada hii ili kuwasaidia wanandoa na wanandoa watarajiwa kufahamu namna ya kutatua na kutawala migogoro yao ya ndoa pale inapojitokeza.

**Ni sawa wanandoa kugombana?**

Inawezekana jibu la watu wengi likawa ni hapana, kwa mtazamo kwamba, kugombana ni jambo baya. Hata hivyo, wataalam wengi wa saikolojia wanasema, migogoro ya hapa na pale katika ndoa ni jambo la kawaida na dalili ya kujali, kukua na kukomaa kwa uhusiano.

Kimsingi, tatizo siyo kugombana, bali namna wanandoa wanavyogombana na kutawala mgogoro wao. George R. Bach na Peter Wyden katika kitabu chao: "The intimate Enemy: How to Fight in Love and Marriage", wanasema, "We have discovered that couples who fight together are couples who stay together-provided that they know how to fight properly".

Kwa tafsiri kwamba, wanandoa wanaogombana ni wanandoa ambao huishi pamoja- pale wanapojua namna bora ya kugombana. Namna bora ya kugombana ni pamoja na kujua kutawala mgogoro. Ifahamike kuwa, ndoa zilizodumu ni zile ambazo, changamoto zilipotokea wanandoa walizikabili pamoja kwa umoja.

Migogoro ni hali halisi na sehemu ya maisha ya binadamu. Katika maisha iko migogoro ya kawaida, kwani watu wanapoishi pamoja, hutokea hali ya kutofautiana hapa na pale. Hali kadhalika, ipo migogoro iliyopitiliza ya mara kwa mara, ambayo huondoa kiwango cha uvumilivu na kuvuruga uhusiano wa wanandoa. Migogoro ina faida na athari zake kama ilivyojadiliwa katika sehemu inayofuata.

**Faida na athari za migogoro ya ndoa**

Migogoro inaweza kujenga ama kubomoa ndoa kama inavyoelezwa katika sehemu hii.

**Faida za migogoro**

Migogoro inaweza kuwa na faida ikishughulikiwa vizuri na mapema. Hata hivyo, faida za migogoro ni chache zaidi kuliko athari zake. Zifuatazo ni faida za migogoro ya ndoa:

- Husaidia wanandoa kufahamiana vizuri zaidi (mazuri na upungufu wao);
- Huwasaidia wanandoa kujua namna ya kuchukuliana;
- Huchangamsha akili na kuimarisha uhusiano wa wanandoa;
- Husababisha matengenezo na kuboresha uhusiano.

**Athari za migogoro ya ndoa**

Migogoro inaweza kuwa na athari kubwa inapotokea mara kwa mara na isiposhughulikiwa kwa makini na kwa wakati. Athari zake haziwahusu wanandoa wenyewe tu, bali na watoto waliozaliwa katika ndoa hizo na familia wanazotoka wanandoa wenyewe kwa ujumla.

**Zifuatazo ni athari za migogoro ya ndoa:**

- Huvuruga ustawi na maendeleo ya familia kwa sababu muda mwingi unatumika kufikiria matatizo badala ya mambo ya maendeleo.
- Huua upendo na kuondoa hisia za mapenzi kwa sababu akili inakuwa imevurugwa.
- Huleta msongo wa mawazo kwa sababu ya kukosa amani na furaha moyoni. Nafsi ya mtu inakuwa imejeruhiwa na kuumizwa. Mtu anaathirika kisaikolojia, kiroho, kimwenendo na kimwili. Afya inadorora na uchumi nao unaugua.
- Hupunguza ufanisi wa utendajikazi.
- Ni chanzo kimojawapo cha ongezeko la wazazi wasio na wenza (single parents hasa (single mothers) nchini, hasa pale ndoa inapofikia hatua ya kuvunjika. Hii ni changamoto kubwa inayoikabili jamii kwa sasa.
- Kuzalisha na kutengeneza familia na jamii ya watu wenye roho ya visasi, visirani, kutelekeza, kuacha na kuachika.
- Mmomonyoko wa maadili. Migogoro ya wazazi huvuruga na kubomoa watoto. Watoto wanakosa malezi bora. Watoto wanajifunza mambo hasi zaidi kuliko mambo chanya kutoka kwa wazazi wao. Hali hii huathiri sana makuzi yao. Watoto wanakosa haki yao ya kufurahia maisha na kumfurahia baba na mama.
- Husababisha vitendo vya ukatili kwa watoto.
- Husababisha ongezeko la watoto wa mitaani na wanaoishi katika mazingira magumu.
- Huleta uadui na kuondoa uwepo wa Mungu na Baraka.

Kutokana na athari hizo, upo umuhimu mkubwa kwa wanandoa kujifunza namna bora ya kutatua na kutawala migogoro yao ya ndoa. Elimu hii itapunguza ukali wa migogoro na athari zake.

Toleo lijalo, tutajadili kanuni 10 za utatuzi na utawala wa migogoro ya ndoa.

- ***Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.***

# MAISHA

Februari 7, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili





Ukurasa 12



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Jinsi ya kung'arisha dirisha

## Juisi ya Malimao

Ukurasa 14



# PARACHICHI

## Tunda linalonogesha, kung'arisha wanawake



Ukurasa 14

# Muulize mwanao amepata wapi penseli mpya?

**Na Moses Ismail**

ALIPOKUWA mtoto wa miaka minne, alipoanzishwa shule ya awali (vidudu), alikuwa na tabia ya kurudi na penseli ya ziada kwenye mkoba wake wa daftari na vitu vingine ambavyo si vyake.

Wazazi hawakuwai kumuuliza ametoa wapi penseli hiyo na hata aliporudi na 'toi' ya gari isiyokuwa yake pia walinyamaza bila ya kuuliza alikoitoa. Maisha yake yakawa ya namna hiyo siku zote.

Utata ulianzia alipoanza shule ya sekondari, huko ndipo zilipoanza kesi za kuwaibia wenafunzi wenzake vitu na kila wazazi wake walipofikishiwa mashitaka yake, walibaki kumwambia: "Angalia, wizi wako, utafungwa."

Leo hii mwizi, anafahamika mtaani na kila akipiti watu huacha shughuli nyingine na kumwangalia kwa makini mpaka anapotokomoea kwenye eneo lao.



Ameshakwapua sana masufuria na hata kandambili kwenye majumba ya watu, sasa hivi kuna tetesi kuwa anaiba simu na vitu vingine majumbani mwa watu kwa kukata nyavu za madirisha ya nyumba.

Kinachowashangaza watu mtaani kwao ni wapi alijifunza tabia hiyo ya wizi wakati wazazi wake si watu wenye tabia mbaya na wanaheshimika katika jamii. Ametoa wapi tabia hii ya wizi?

Mara kadhaa wazazi wake waliposikia anakwapua vitu majumbani mwa watu, wakati ule akiwa mtoto wa miaka 15, walishangaa na wakati mwingine walihisi anasingiziwa. Wakajiuliza; "ametoa wapi tabia hizo?"

Kwa sababu sasa hivi ni mtu mzima, mwenye zaidi ya miaka 20, hawana tena la kumfanya kwa sababu tayari wamemfukuza nyumbani na hawataki tena kusikia habari zake kwa sababu ya tabia zake za wizi.

Wamefanya hivyo kwa sababu ya kulinda heshima yao mtaani, wanasema: "Hatuwezi kuishi na mtoto mwizi kama wewe. Unatutia aibu. Katafite wazazi wako, sisi si wazazi wako."

Sasa wazazi wake wanamfukuza nyumbani eti kwa sababu ni mwizi na anawatia aibu? Ni ujasiri gani wanaoutumia wazazi hawa kumfukuza nyumbani eti kwa saabu hawawezi kuwa na mtoto mwizi kama yeye?

Iwapo wazazi wangemuuliza mapema amepata wapi ile toi ya kigari, iwapo wangemuuliza juu ya lile lundo la penseli na pia yale madaftari ya mwaka mzima, pengine leo asingekuwa mwizi au kibaka kama alivyo sasa.

Kufumbia kwao macho mambo hayo ndiko kulikomfanya awe mwizi wa sasa. Ndio, ni mwizi na ni mtoto wenu na mnawajibika kwa wizi wake, mlimsaidia kujenga tabia hiyo tangu akiwa mdogo.

## QUIZ

**NA HAMIS KIDAGO**
0657 207168

### LE QUIZ DU WEEK


Le Verbe Suivre – Kitenzi "Fuata"

1. Kamilisha unyumbuaji wa kitenzi "Fuata" katika nyakati mbalimbali kama zilivyoainishwa hapo chini.

Indicatif
present
je ………………………
tu ………………………
il/elle ………………………
nous ………………………
vous ………………………
ils/elles ………………………
imparfait
je ………………………
tu ………………………
il/elle ………………………
nous ………………………
vous ………………………
ils/elles ………………………
futur simple
je ………………………
tu ………………………
il/elle ………………………
nous ………………………
vous ………………………
ils/elles ………………………
passé simple
je ………………………
tu ………………………
il/elle ………………………
nous ………………………
vous ………………………
ils/elles ………………………
passé compose
j' ai ………………
tu as ………………
il/elle a ………………
nous avons ………………
vous avez ………………
ils/elles ont ………………
plus – que – parfait
j' avais ………………
tu avais ………………
il/elle avait ………………
nous avions ………………
vous aviez ………………
ils/elles avaient ………………
futur anterieur
j' aurai ………………
tu auras ………………
il/elle aura ………………
nous aurons ………………
vous aurez ………………
ils/elles auront ………………
passé anterieur
j' eus ………………
tu eus ………………
il/elle eut ………………
nous eumes ………………
vous eutes ………………
ils/elles eurent ………………
Conditionnel
present
je ………………
tu ………………
il/elle ………………
nous ………………
vous ………………
ils/elles ………………
passé
j' aurais ………………
tu aurais ………………
il/elle aurait ………………
nous aurions ………………
vous auriez ………………
ils/elles auraient ………………
Infinitif
present
………………
passé
………………
Participe
present
………………
passé
………/………
………/………
………………
Imperatif
present
………………
………………
………………
passé
………………………
ayons ………
………………………
Subjonctif
present
que je ………………
que tu ………………
qu' il/elle ………………
que nous ………………
que vous ………………
qu' ils/elles ………………

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO

**NCHINI Marekani mtoto anapokwenda kulala, mama humwambia "Goodnight baby boy"**

**Kule Uingereza wazazi humwambia mtoto, "sweet dreams baby boy"**

**Uhispania wanapoenda kulala humtakia mtoto wake "goodnight my baby"**

**Tanzania mtoto anapokwenda kulala, mama humuuliza "umeshajisaidia? Haya kalale na ukichafua kitanda utakoma,"**



**Mto pangani unapatikana mkoa gani?**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Je, maisha yako yanaongozwa na nguvu gani?

KARIBU tena msomaji wangu tujadili masuala mbalimbali kuhusu maisha kupitia safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo hebu mada yangu ijikite katika mfumo wa swali. Huu ni mwaka 2021. Je, unajua nini kinaongoza maisha yako mwaka huu?
Siku zote, kile ulichodhamiria ndicho kitakachotokea. Huwezi kwenda zaidi ya mawazo uamuzi yako. Ni rahisi mume au mke kumwambia mwenzake, 'wewe huna uamuzi".
Maamuzi ni nini? Ni uwezo wa mtu au hatua anayochukua mtu kufanya jambo fulani, liwe zuri au liwe baya. Uamuzi wa kuchukua hatua itategemea uamuzi atakaochukua mtu.
Na ili kufanya jambo lolote, itategemea uamuzi uliyonao katika kulifanya.
Wapo watu wengi ambao hupania kutekeleza mipango mbalimbali lakini wanachelewa kwa kutokuwa na uamuzi. Kwa mfano, ulipanga kumuoa binti fulani au kuolewa na fulani, lakini unakuta ameshachukuliwa na mtu mwingine , kisa umechelewa kuamua. Muujiza wako unao wewe mwenyewe.
Wapo wanadamu ambao maisha yao yanaongozwa na Mungu, ambapo wengine wanaongozwa na nguvu za giza(ushirikina). Jiulize, maisha yako yanatawaliwa na nguvu gani?
Zaidi ya hapo, wapo watu wanaoongozwa na jambo fulani lililotokea huko nyuma. Wengine wanaongozwa na matatizo yaliyowapata, majeraha yaliyowahi kuwapata. Wengine chuki iliyowapata na hasara. Wengine wanaongozwa na hatia, imani mbaya na hofu mbaya (ipo pia hofu nzuri).
Watu walio wengi wanaongozwa na vitu vifuatavyo. Leo nitazungumzia HATIA, wiki ijayo tutaangalia CHUKI. Kuna watu wanaongozwa na hatia.
Mtu anayeongozwa na hatia hutumia muda mwingi kuepuka lawama. Hapendi kulaumiwa, hivyo atafanya kila jitihada kuhakikisha hapati lawama.
Mtu wa aina hii, maisha yake yanaongozwa na hatia. Kila wakati anasikia hatia moyoni mwake. Akisikia lawama, utamsikia akisema mimi sipo. Mtu huyu huongozwa na mambo mabaya yaliyotokea nyuma.
Kutokana na mambo yaliyopita, anaruhusu moyo wake utawaliwe na mambo hayo. Yaani mambo ya jana ndiyo yanayomtawala leo.
Inawezekana ni mtu anayefanya biashara akapata hasara. Leo hataki tena kufanya biashara kwa kuogopa kupata hasara. Inawezekana aliahidiwa pale kazini kupewa cheo fulani.
Kile cheo kinamsababishia usumbufu mwingi na lawama nyingi zinakuja kwake. Kwa hiyo anaanza kusema sitaki tena hicho cheo, anaogopa lawama. Maisha Ndivyo Yalivyo.
Yupo mwalimu mmoja aliwahi kuniambia kwamba shule kwao, wenzake walikuwa wanakwepa Ofisi ya Taaluma. Kisa wanafunzi wakifeli, wewe ndiye wa kwanza kujieleza. Utaeleza kwanini wamefeli. Hakuna mtu aliyekuwa anataka lawama.
Hao walikuwa wanaongozwa na hatia. Kila mtu hajiamini. Mtu wa aina hii ni mtu ambaye anaruhusu hasara ya jana yake iharibu faida ya leo na kesho. Hawezi kufanya chochote maadam tu alipata hasara.
Unakuta ni binti anasema hataki tena kuolewa kwa sababu alichumbiwa, akaumizwa. Kwa hiyo maumivu ya mwanaume aliyemlaghai, leo hii yamemfanya akose mwanamume sahihi wa kumuoa tena.
Inawezekana alichumbiwa akaanza kupeleka zawadi, akamnunulia nguo, vyombo na kadhalika, lakini akaishia machungu. Binti mmoja akamfuata baba yake mmoja wa kiroho kutaka ushauri.
Akamwambia, "unamjua kijana fulani? Huyo alinichumbia. Nimempa fedha zangu nyingi. Mara ya mwisho nilimpa Sh. 50,000. Lakini mbaya zaidi alikuja kwangu nikampa Biblia yangu. Sasa baba yangu wa kiroho nataka anirudishie Biblia yangu na zile Sh. 50,000 zangu!"
Kwa kumtizama huyo binti, utagundua kwamba anaongozwa na hatia. Ndani yake yaliyomtokea jana yanamfanya akose ya leo na kesho. Ni tatizo linalosumbua familia nyingi.
Wanandoa wengi wamejikuta wakiachana kutokana na kuwekeana mafundo mioyoni mwao. Bado wanakumbukia ya zamani wakati wanaoshi leo. Wanasahau kwamba ya kale yameshapita tazama yamekuwa mapya!
Usisumbukie historia ambayo haikusaidii leo. Angalia zaidi kilichoko mbele yako. Makosa yapo na ipo nguvu ya kusameheana pia. Unapotunza maumivu ya jana moyoni, yatazuia au hata kuchelewesha mafanikio mazuri huko uendako.
Msomaji wangu, tiishie hapa kwa leo. Wiki ijayo tutajadili chuki inavyoweza kumletea mtu madhara kimaisha. Bila shaka lipo jambo umeweza kujifunza kwa habari ya hatia. Je, unayo maoni, ushauri au kisa cha kimaisha? Nitumie ujumbe mfupi kupitia 0715268581.

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Umakini unavyohitajika matumizi dawa za asili

MATUMIZI ya dawa za kienyeji yameongezeka kwa kuwa kila mtumiaji anataka kujiponya dhidi ya changamoto za upumuaji, nimonia au maradhi mengine ya mfumo wa upumuaji, ikiwa ni pamoja na kuimarisha kinga ya mwili katika kukabiliana na maradhi mbalimbali.
Kwa sasa wapo wanaotumia mchanganyiko uliotengenezwa na Taasisi ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), na Shirika la Maendeleo ya Viwanda (TRIDO) na nyingine ambazo zimesaidia wengi.
Aidha, Rais John Magufuli, alieleza huwa dawa hizo zimethibitika kutibu kwa asilimia 99.9, na kutaka Watanzania kutozipuuza bali kuzitumia ipasavyo katika kutibu magonjwa mbalimbali kwa kuwa dawa za asili siku zote ni nzuri.
Pia, wengine wanatengeneza mchanganyiko wa mimea mbalimbali, huku katika maduka ya dawa za kienyeji kukiwa na aina tofauti tofauti za dawa zinazowasaidia wengi katika changamoto za kupumua.
Wapo ambao wamejikuta wanatumia dawa za hospitali, mchanganyiko wa kienyeji jambo ambalo linapaswa kuangaliwa kwa kuwa kitaalam matumizi ya madawa mengi huichosha figo na ni rahisi kusababisha madhara makubwa ya kiafya.

Baadhi wanakunywa pasipo kufuata kipimo cha kitaalam na hasa kwa dawa za kienyeji ambazo mtu hujipimia mwenyewe na hasa kwa zile zinazoelezwa kuwa ni tiba lishe, na huku akitumia za hospitalini.
Tanzania siyo kisiwa kwa kuwa nchi zote zinazoizunguka zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa na ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona, basi ni muhimu kuchukua tahadhari ikiwa ni pamoja na kula vyakula vitakavyoimarisha kinga ya mwili.
Ni muhimu kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi sahihi ya dawa hizo, vinginevyo kuna hatari ya miaka ya baadaye watu kuelemewa na magonjwa ambayo pengine tiba yake inaweza kuwa ya gharama kubwa.
Kuwapo na taratibu za kuelimisha wananchi juu ya matumizi ya dawa hizo, hususan wakati huu ambao wengi wanapambana kujitibu kwa namna tofauti tofauti.
Ni muhimu kuwapo kwa vipindi kwenye luninga, mtandaoni na magazetini ili kuafikia wananchi wengi kwa namna tofauti, kukabiliana na changamoto za upumuaji na nimoni.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatakiwa kuhamasisha wananchi kutumia dawa hizo kwa uangalifu, kwa kupitia mbinu mbalimbali za utoaji elimu kama kuwa na vipindi maalum na vipeperushi ili kusidia jamii.
Pia, Baraza la Tiba asili lifuatilie dawa zote zinazotengenezwa sasa na kuelezwa kuwa zinatibu magonjwa ya mfumo wa upumuaji, ili kusaidia wananchi kutumia mchanganyiko wenye vipimo sahihi na kwa wakati sahihi na kuepusha matumizi holela ya dawa hizo.
Unapotumia dawa kwa sasa madhara yake huonekana miaka mingi, pengine kunaweza kuwa na ongezeko la wagonjwa wa wanaotokana na matumizi ya dawa nyingi.
Ninaamini elimu itakayotolewa itakuwa mkombozi kwa wengi hasa maeneo ya vijijini ambako miti ya asili ni mingi, matumizi ya dawa za hospitalini na asili ni kubwa, jambo ambalo litazalisha matatizo mengine baadaye.
Tayari wataalam wamethibitisha dawa hizo kufanya vizuri katika tiba za mfumo wa upumuaji, nyingi zikiwa za kunywa na kufukiza.
Pamoja na kuendelea kujitibu ni muhimu sana kuendelea kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka, kutakasa mikono kwa sanitaiza, kuepuka kushika macho, mdomo na pua, kuepuka misongamano na kuvaa barakoa mara unapokuwa kwenye mkusanyiko.
Yote haya yatasaidia kuleta matokeo chanya kwa wengi na kuendelea kuwa na nguvu kazi sahihi kwa taifa, vinginevyo itapungua na kumalizika kama ilivyo kwa nchi ambazo corona imewaathiri kwa kiasi kikubwa.

**Mungu ibariki Tanzania**

# Aina ya magauni ya harusi yanayofaa kuvaliwa



# MITINDO



# 'SUSPENDERS' MIKANDA INAYOKUPA RAHA TELE

JE, umewahi kumuona yule mtangazaji maarufu wa marekani, Larry King, wakati wa enzi zake? Kama umemuona basi vazi lake la mkanda maarufu kama 'Suspender' litakukaa kichwani.

Mkanda huu unaleta ladha ya kipekee kwa wale ambao hawataki kuvaa nguo nzito hasa katika kipindi hiki cha joto.

Suspenders ni kama mkanda wa mwili unao saidia suruwali yako isipwaye na kukufanya utoke mtanashati katika kipidi chote kuanzia asubuhi hadi jioni.

Jambo muhimu pale unavaa mkanda huu, usivae mkanda mwingine kwenye suruwali yako. Tafuta suruwali inayokubana vyema kiunoni, lakini isikubane sana.

Mikanda ya aina hii ipo katika mitindo tofauti, ni chaguo lako tu itakufanya upendeze zaidi.

Wanaopenda kuvaa mikanda ya Suspenders, wengi wao ni vijana, wasanii na watu wenye umri wa kati.

Kulinganisha rangi tofauti ni jambo zuri, lakini usichanganye rangi nyingi.

Kama unapenda kuvaa mavazi za kupooza, mikanda ipo inayofaa kama rangi nyeupe na nyeusi.

Kwa wapenzi wa mashati au fulana za mikono mifupi, wanaweza kutoka vyema wakipigilia mikanda ya aina hii na kutoka matembezini bila hofu.

Sio lazima uvae suspenders na tai suruali ya vitambaa, hata Jeans zinafaa kuvaliwa nazo. Katika kukupatia furaha zaidi tupia na kofia inayoendana na mavazi yako.

Sehemu yoyote unayotaka kwenda. Suspenders haitakufanya uonekane tofauti kimaadili, kwani inafaa harusini, mikutano ya kikazi, ofisini na hata matembezi ya jioni.

UREMBO



# PARACHICHI

## Tunda linalonogesha, kung'arisha wanawake

PARACHICHI ni aina ya tunda ambalo lina maajabu mengi katika urembo na afya ya mwanamke.

Tunda hili ambalo lina utajiri wa virutubisho linapopatikana kwa urahisi hapa nchini.

Wataalamu wa afya wanaamini Parachichi ni bidhaa adimu katika kuujenga mwili na kuuweka katika ubora wake.

Wanasema ukitumia kwa usahihi, unaweza kupata matokeo ya haraka hasa katika utunzaji wa nywele, ngozi, mmeng'enyo wa chakula na macho.

KUNA NINI NDANI?

Ndani ya parachichi kuna kalori inayotokana na mafuta ni 184, miligramu 11 za sodiamu, gramu 13 za wanga na gramu 10 za nyuzinyuzi za lishe.

Aidha, kuna gramu ya moja ya sukari, vitamini K asilimia 26, C asilimia 17, Potasiamu asilimia 14, Vitamini B5, asilimia 14, Vitamini B6 asilimia 13, Asidi ya Folate asilimia 20 na Vitamini E asilimia 10.

FAIDA ZAKE

Endapo utatumia kama chakula au kujipaka mwilini kama 'Scrub' itakurudisha katika hali ya ujana zaidi kwani inaondoa kwa kiasi kikubwa makunyazi.

Pia uji wa parachichi ukipaka kwenye nywele kwa kila wiki, itakupa faida ya kuboresha afya ya nywele zako na kubaki katika rangi ya kung'aa.

Badala ya kununua mafuta kwa gharama kubwa ili kupata vitamini E kwa ajili ya kung'arisha ngozi na nywele zako, basi kula tunda la parachichi kila siku.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# JUISI YA MALIMAO

KINYWAJI hiki ni rahisi kuandaa na ni kizuri kwa afya zetu.

Uwapo wa limao na tangawizi unasaidia mwili kupata virutubisho na vitamini mbalimbali mwilini.

Epuka kutumia sukari nyingi mana si nzuri kwa afya, ukiweza tumia asali kiasi.

Mahitaji

Malimao fresh sita, asali kikombe 1, tangawizi iliyokwanguliwa nusu kikombe, maji vikombe 2 maji ya baridi vikombe 14

Namna ya kuandaa

Chukua bakuli safi, kwenye bakuli kamua malimao kisha toa mbegu zote, yabaki maji ya limao.

Washa jiko, bandika sufuria weka vikombe 2 vya maji, asali na tangawizi.

Acha mchanganyiko uchemke kwa moto mdogo kwa muda wa dakika 10, mpaka asali iyeyuke na harufu nzuri ya tangawizi isikike.

Epua, acha ipoe, chukua jagi safi weka maji ya limao, maji ya baridi vikombe 14 kisha weka mchanganyiko ulioutoa jikoni.

Changanya vizuri weka kwenye jokofu kwa muda wa saa moja.

Kama utapenda weka majani ya mnanaa na giligilani ili kupata harufu nzuri.

Juisi yako itakuwa tayari kwa ajili ya kunywa baada ya kupata mlo wako safi au wakati umepumzika na familia.



# MAISHA NI NYUMBA

## Na Elizabeth Zaya

# JINSI YA KUNG'ARISHA DIRISHA



DIRISHA la kioo ni moja ya vitu vinavyochangia kung`arisha nyumba.

Ili dirisha liendelee kuwa bora na kung`arisha nyumba lazima lisafishwe.

Usipoweka kipaumbele katika jambo hilo usishangae kuona mvuto wa nyumba yako ukaanza kufifia kidogokidogo na mwisho wake ukaichukia nyumba kabisa.

Usafishaji wa dirisha ni lazima uwe na muda maalum ambao hakuna jua kali.

Kwa sababu unaposafisha wakati wa jua kali, maji unayomiminia katika dirisha lako hukaushwa kabla ya kupitisha sponji na hivyo kukuchukulia muda mwingi na pia haliwezi kung`aa vizuri na huacha ukungu.

Wakati unasafisha unatakiwa uwe pia na dawa maalum au kama unatumia maji si vibaya ukadondoshea kidogo vitone hata viwili vya maji spesho yenye mchanganyiko wa limao, maarufu kama 'vinegar'.

Baada ya hapo unalowanisha 'sponji' yako ama kitambaa laini kwa kuchovya kwenye maji hayo na kuanza kusafisha katika dirisha lako.

Hakikisha unasafisha kuanzia juu kushuka chini, ili uchafu wote utiririkie kwenda chini na kukuhakikishia kuwa hakuna uchafu utakadondokea kwenye sehemu ambayo imeshasafishwa tayari.

Kama eneo la dirisha unalotaka kusafisha ni chafu sana ama kuna vumbi jingi au utando wa buibui, futa kwanza kwa kitambaa kikavu kabla ya kusafisha na maji.

Uwe makini kuchunguza uchafu uliopo kwenye kona za madirisha yako.

Epuka kuweka maji mengi kwenye sponji ama kitambaa unachotumia kusafisha ili yasimiminikie chini sehemu ambayo siyo ya dirisha iwe ukutani ama sehemu nyingine isiyohusika.

Hakikisha unasuuza na kukausha dirisha lako kwa kutumia kitambaa kikavu na laini na baada ya hapo rudia tena kwa ajili ya kuling`arisha.

Kama utakuwa na dawa maalum ya kusafishia itapendeza zaidi kuipulizia kidogo katika dirisha huku ukifuta kwa kutumia kitambaa cha pamba ambacho hakitoi nyuzi.

Hakikisha dawa unayotumia kusafishia ni ile ambayo haiwezi kuharibu ama kupausha mbao za dirisha lako.

Kama dirisha lako ni la kioo, hakikisha sponji ama kitaamba ulichotumia kusafishia kioo ni tofauti na kile unachosafishia kwenye flemu ama kona za dirisha lako.


Katika maeneo ya flemu na kona, safisha kwa kutumia kitambaa kigumu zaidi ambacho kitabeba uchafu wote kwa sababu eneo hilo huhifadhi uchafu mwingi.




# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU ZA KUPAMBA CHUMBA CHAKO CHA KULALA ILI KIONEKANE NA MVUTO WA KIPEKEE

1: Tambua mtindo unaotaka kuutumia kupamba meza yako ya pembeni, ukifahamu utaweza kubuni muonekano mpya wa chumba chako.
2: Ng'arisha kwa kuweka taa ya mezani pembeni ya kitanda, licha ya kupamba taa zinasaidia kutoa mwanga kama una tabia ya kuamka usiku.
3: Weka picha ukutani ili iwe kumbukumbu au pambo litakalokufanya uwe mtulivu.
4: Weka trei ndogo kwa ajili ya kuweka vitu vidogo vidogo pembeni ya kitanda chako. Trei ndogo ni timilifu kwa kutumia kupangia vitu kwenye meza ya pembeni mwa kitanda.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
'NIMEDAMSHI' SEMENI KINGINE
BARABARA
INAMAANA NYIE WAPANGAJI HAMPO AU MMEAMUA KUFANYA MGOMO BARIDI?...TUNATIANA NJAA!
DALALI
VYUMBA VIPO BWELELE
WEWE SI MBISHI?... NINI KILICHOKU-FANYA UVAE...
AIBU...
TUCHUKUE TAHADHARI TUSIPUUZIE
ONENI HUU MSONGAMANO WALA HATUJALI!
MNAZUNGUMZIA TAHADHARI IPI? DEREVA ANAVYO-TUPAISHA AU IPI?
KABISAA!
ACHENI UMBEA VAENI BARAKOA
KUMBE MZITO! INGEKUWA KILA SIKU NINGEPINDA MGONGO
MIE MBONA SILALAMIKAGI?
MIMI POMBE BASI...
KWANI HAPA NIMEKUNUNULIA POMBE AU BIA?
MIMI NA PESA YANGU, UNA-MPENDA NANI?
NIKITOA JIBU UTASTA-HIMILI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KUTELEZA NDIO MWENDO WA NYOKA...

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaunga mkono Afrika kuongoza WTO

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS Joe Biden amemaliza mgogoro kuhusu uteuzi wa mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), baada ya kuamua kumuunga mkono aliyekuwa waziri wa fedha wa wa Nigeria, Ngozi Okonjo-Iweala.

Ngozi alikuwa anaongoza miongoni mwa wagombea waliokuwa wanawania wadhifa huo hadi mwezi Oktoba, lakini utawala wa Trump, ulimzuia kwa kueleza hau-muungi mkono, badala yake unataka mwanamke mwingine kutoka Korea Kusini, Too Myung-hee.

Kutokana na msimamo huo, Too Myung-hee amejiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Ikiwa atathibitishwa, Dkt. Okonjo-Iweala atakuwa mwanamke wa kwanza mwafrika, kuongoza shirika la WTO.

Dkt. Okonjo-Iweala alimsifu mpinzani wake kwa ujumbe wake aliotoa wa maridhiano.

"Kuna kazi muhimu mbele yetu inayohitaji ushirikiano wetu pamoja." Alisema.

Kamati ya uteuzi ya WTO, iliyoketi mwezi Oktoba ilipendekeza wanachama wake 164 kumteua Dkt. Okonjo-Iweala kuchukua nafasi ya kiongozi anayeondoka Roberto Azevedo.

BBC



Kiongozi mpya wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iwealai **(PICHA: BBC)**

## Jeshi laamuru kuzimwa Twitter na Instagram

**NAYPYIDAW, Myanmar**

UTAWALA mpya wa kijeshi nchini Myanmar, umeziamuru kampuni za mawasiliano nchini humo kuifunga kwa muda mitandao ya kijamii ya Twitter na Istagram.

Hatua hiyo imekuja siku chache tangu ilipoweka vizuizi kama hivyo kwa mtandao wa Facebook.

Kulingana na tovuti moja ya habari, Jeshi limezitaka kampuni za simu kuzuia upatikanaji wa mitandaoni hiyo kuanzia usiku wa kuamkia jana ikisema inatumika kuvuruga uthabiti wa taifa hilo.

Amri hiyo kutoka wizara ya uchukuzi na mawasiliano ilitolewa katika wakati idadi ya watu waliojaa hasira ikiongezeka tangu jeshi lilipofanya mapinduzi siku ya Jumatatu na kuuondoa madarakani utawala wa kiraia. Miito ya kuitisha maandamano na kuwataka raia kutoutiii utawala wa kijeshi imeendelea kusambaa mitandaoni tangu jeshi lilipowakamata viongozi wa serikali akiwamo kiongozi wa kiraia Aung San Suu Kyi.

**DW.**

## Mazungumzo kutafuta suluhu yavunjika

**MOGADISHU, Somalia**

MAZUNGUMZO ya dharura baina ya viongozi wa kisiasa walio kwenye mvutano nchini Somalia, yamemalizika bila ya kufikiwa makubaliano.

Mkutano huo ulikuwa maalumu kwa ajili ya majadiliano ya jinsi ya kuendelea na uchaguzi mkuu siku chache kabla ya kufikia mwisho wa muhula wa Rais aliye madarakani. Waziri wa Habari wa nchi hiyo, Osman Dubbe, aliwaambia waandishi habari mjini Mogadishu kuwa serikali ilitoa nafasi ya kufanyika majadiliano na kumaliza tofauti zilizopo, lakini baadhi ya wanasiasa wamekataa uwezekano wa kufikia suluhu.

Kutokana na hali hiyo, huenda Somalia itashindwa kumchagua rais mpya kabla ya Februari 8.

Mazungumzo kati ya serikali kuu na viongozi wa serikali za majimbo yalivunjika kutokana na misimamo tofauti kuhusu utaratibu wa kufanyika uchaguzi huo.

Mkwamo huo unatishia kuzuka kwa mzozo wa kikatiba kwenye taifa hilo.

**DW**

# ICC kuichunguza Israel uhalifu wa kivita

**THE HEGUE, Uholanzi**

HATIMAYE majaji wa Mahakama ya Kimataifa ua Uhalifu (ICC) wamekubaliana chombo hicho kinaweza kuchunguza vitendo vya kihalifu vilivyofanywa katika maeneo ya Gaza, Ukingo wa Magharibi na Jerusalem Mashariki.

Hata hivyo, Israel ilipinga hatua hiyo kwa kueleza ni ya kisiasa zaidi, huku Wapalestina walisema ni sehemu ya ushindi dhidi ya unyanyasaji unaofanywa na jeshi la Israel.

Katika hukumu iliyotolewa siku ya Ijumaa, Mahakama hiyo iliamua inayo mamlaka ya kisheria kwenye maeneo ya Palestina yanayokaliwa kimabavu na Israel tangu vita vya mwaka 1967.

Uamuzi huo uliofikiwa na majaji wawili kati ya watatu wa Mahakama hiyo. Kutokana na uamuzi huo, sasa inaweza kufunguwa njia kwa mwendesha mashitaka mkuu wa mahakama hiyo, kufunguwa uchunguzi wa uhalifu wa kivita dhidi ya vitendo vya jeshi la Israel.

Mwaka 2019, mwendesha mashitaka huyo, Fatou Bensouda, alisema kulikuwa na sababu za kutosha kufunguwa uchunguzi huo dhidi ya vitendo vya jeshi la Israel katika vurugu zilizotokea Ukanda wa Gaza mwaka 2014.

Alivitaja vikosi vya Jeshi la Ulinzi na Israel na makundi yenye silaha ya Palestina, kama vile Hamas, kuwa wanaweza kuhusika na vitendo hivyo.

Mapigano hayo ya mwaka 2014 yalipoteza maisha ya Wapalestina wanaokaribia 2,000 na Waisraeli 60.

Mwanasheria huyo alitaka kuchunguza makazi ya walowezi wa Kiyahudi katika eneo la Ukingo wa Magharibi, lakini kwanza aliiomba Mahakama hiyo kuamuwa endapo anayo mamlaka ya kisheria ya kuendelea na kesi hiyo.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amelaani uamuzi huo, akiita Mahakama hiyo kuwa chombo cha kisiasa na sio taasisi ya kisheria.

"ICC inapuuzia uhalifu wa kweli wa kivira na badala yake inaiandama Israel, dola ambayo ina serikali imara ya kidemokrasia inayoenzi utawala wa sheria," alisema Netanyahu.

Waziri wa Masuala ya Kiraia wa Palestina, Hussein al-Sheikh, aliupongeza uamuzi huo na kuuita kama ushindi kwa ukweli, haki, uhuru na maadili ulimwenguni.

Israel, ambayo si mwanachama wa ICC, imekuwa ikihoji Mahakama hiyo kuwa haina mamlaka yoyote ya kisheria kufanya uchunguzi huo.

**DW.**

SAFU

# Siku ya kifo changu ni nani atakayenililia?



Na Magabilo Masambu

UKOMO wa maisha ya mwanadamu umeelezwa katika vitabu mbalimbali vya dini na vya kidunia (sayansi) kwamba mwanadamu atazaliwa lakini siku moja atakufa na kutoweka duniani.

Lakini baadhi vitabu vya dini vinaeleza juu ya uwapo wa maisha mengine baada ya kifo. Hii ina maana kwamba hakuna mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke atakayeishi milele.

Kila mmoja wetu yuko duniani kwa kusudi maalumu pamoja na kwamba inawezekana ukazaliwa, ukaishi na ukaondoka bila kufahamu kusudi la kuwapo duniani. Hivyo kila mmoja wetu aliye hai anayo kazi ya kutafuta kusudi la kuwapo duniani.

Wakati tunaendelea kuishi ni muhimu sana kila mmoja wetu kujiuliza "Siku ya kifo changu ni nani atakayenililia? Maisha yana maana tuwapo hai lakini yana maana zaidi kama tutayagusa maisha ya watu wengine. Duniani tumeumbwa ili tutegemeane, pengine tungekuwa kila mmoja wetu amejitosheleza kwa kila kitu, inawezekana maisha yangekosa maana.

Pamoja na kuhangaika juu ya maisha yetu binafsi, ni muhimu sana kujiongezea idadi ya watu watakaokulilia kwa dhati siku ya kifo chako. Hii ina maana gani hasa? Kila mmoja wetu akiwa na fikra hizo basi upendo miongoni mwetu utaongezeka maradufu na maisha yatakuwa na maana zaidi.

Tunahangaika sana juu ya kujenga vitu duniani. Si jambo baya lakini ni rahisi sana kumbukumbu kubakia kwa watu uliyogusa maisha yao, kuliko majengo na mali nyingi utakazokuwa umeziacha. Wakati mwingine mali utakazoziacha zinaweza kuwa vyanzo vya migogoro mikubwa. Simaanishi tusiwekeze lakini tukiwekeza katika maisha ya watu, utakuwa uwekezaji utakaoacha alama kama wasemavyo siku hizi.

Unaweza kuwa na madaraka, mali, fedha na vitu vinginevyo vya namna hiyo lakini vyote hivyo ni vya kupita. Ukifanikiwa kuwa navyo basi uvitumie kuleta furaha kwa watu wengine ambao kwa hakika hata siku haupo watabaki kukumbuka kwamba ulikuwapo.

Mark Cahill katika kitabu chake kinachoitwa "One Heartbeat Away" anauliza When you die, what do you think will be on the other side? Akimaanisha wakati utakapokufa, unafikiri ni nini kitakuwa upande wa pili? Kwa maana ya maisha baada ya kifo.

"Msistaajabie maneno hayo, kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliyomo makaburini wataisikia sauti yake, nao watatoka.Wale waliyofanya mema kwa ufufuo wa uzima na wale wliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu (Yohana 5:28-29). Unaposhindwa kutengeneza watu watakaokulilia kwa kutokuwepo kwako maana yake, kuna uwezekano mkubwa unatengeneza watu watakaofurahia na kusherekea siku haupo. Tafasiri yake unawatendea mabaya watu hao.

Natambua kwamba si kila utakayemtendea mazuri atakushukuru na kuona umuhimu wako, lakini miongoni mwa wabaya hawakosekani wema, ambao watasema bila fulani nisingefika hapa nakadhalika.Lakini hatupaswi kukata tamaa kwa sababu kuna muda unaweza kuwasaidia watu wakati ambao hawana uhitaji bali siku uhitaji huo utakapowapata, watakumbuka na misaada ya nyuma, hapo ndipo watakapokulilia wakati haupo.

Wakati mwingine hata baadhi ya unaowasaidia wanaweza kugeuka na kuwa adui zako, wanakusema vibaya kwa watu, wanakufitini hii ni kwasababu ni vigumu sana kutambua mchango wa mtu akiwapo, bali atakapoondoka ndipo pengo lake litakapoonekana. Pengo hilo maranyingi ndilo linalowafanya watu walie sana siku ya msiba na pengine maisha yao yote.

Adui wa binadamu si wanyama wa mwituni tu bali ni binadamu mwenyewe. Dunia hii itakuwa salama tu pale kila mmoja wetu atakapotenda wema kwa mwenzake. Ubaya wa wengine husababishwa na ubaya wetu pia kwa sababu kama binadamu anaweza kujifunza wema anaweza kujifunza ubaya pia. Kama huna uwezo wa kuwasaidia basi angalau usiwaumize.

Pengine nisieleweke kwamba wenye uwezo wa kusaidia wengine ni wale wenye mali nyingi, au madaraka makubwa hapana vitu unavyoviona kwamba ni vidogo kwako, ndivyo vinavyogusa maisha ya wengi. Kuna mtu anaweza kukosa Sh. 100 ili iwe 400 apande daladala, unaweza kuona ni kitu kidogo sana lakini hiyo Sh. 100 itamfikisha nyumbani na atakushukuru sana maishani.

Mwisho ni bora kuwa na watu wengi watakao kulilia na kukushukuru maishani kuliko mali na madaraka yasioishi.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***ARUSHA-TANZANIA***

# Unayakumbuka wanasesere, magari ya maboksi?



Na Adam Fungamwango

UKIANGALIA kwa sasa vitu vingi vya kuchezea watoto ni vya kutoka nje ya nchi, vilivyotengenezwa viwandani. Utakuta watoto wa kike na wa kiume wakichezea magari, pikipiki,kwa watoto wa kiume na midoli kwa watoto wa kike.

Hivi sasa wazazi wamekuwa wakiwanunulia watoto wao vitu vya kuchezea ili kuwafanya wawe na furaha, wapate burudani na wakati huo huo wajifunze vitu fulani au kujua vipaji vyao kupitia vitu hivyo vya kuchezea.

Hiki ni kizazi cha watoto wa sasa, ambacho wengi wao ni wapole, watulivu na wenye akili nyingi.

Na hii inatokana kuwa kuzaliwa kwenye kizazi ambacho teknolojia imetamalaki na kuwa ni maisha ya kila siku.

Mtoto anazaliwa anaikuta televisheni, simu na baada ya miaka kadhaa tayari anaanza kuichezea na kujua kila kitu kilichomo kwenye simu na matumizi yake wakati mwingine kuliko hata wazazi wake.

Lakini tatizo la watoto wengi wa kisasa ni kwamba si wabunifu. Wamekuwa na akili nyingi za darasani, lakini hawawezi kubuni au kutengeneza kitu. Kwa kifupi ni kwamba wengi hawawezi kazi za mikono. Wanashindwa kuitoa akili yao kichwani na kuileta kwenye mikono yao kufanya jambo ambalo litakuwa na faida kwao, wazazi wao, eneo linalowazunguka na taifa kwa ujumla.

Ndiyo maana kwa sasa vijana wengi wanalalamika kuwa hakuna ajira. Ni kweli ajira zimekuwa za tabu, lakini tatizo ni kwamba kila kijana sasa anataka awe anakaa ofisini.

Kumekuwa kuna kutupiana mpira, serikali ikisema tatizo ni kwamba vijana wengi wa sasa hawaajiriki kwa sababu wanashindwa kufanya kazi ambazo wameziomba, lakini baadhi ya wazazi wakishangazwa na vijana wao kushindwa kujitegemea kama ilivyokuwa wao zamani.

Wazazi wanachoshangaa ni kwamba umri ambao wao walikuwa tayari walikuwa wameshaondoka kwa wazazi wao kwenda kujitegemea, vijana wao hawana hata dalili ya kuondoka.

Tena siyo kuishi tu nyumbani, lakini wakiwategemea wazazi wao kwa asilimia 90 ya mahitaji kama vile malazi, chakula, matibabu, labda kwa mbali kwenye mavazi

Hebu tuwaangalie watoto wa zamani ambao wengi wao hawakuwa na akili sana ya darasani, lakini walikuwa watundu, wenye uthubutu, na wabunifu.

Kwanza walikuwa hawachezei vitu vya kununuliwa na wazazi wao. Si mwamba hawakuwa na uwezo tu, lakini pia havikuwapo.

Watoto wa wakati huo walikuwa wakitafuta maboksi ambayo yalikuwa wametupwa wenye maduka baada ya bidhaa zilizohifadhiwa humo kumalizika.

Baada ya kuokota, wanayakatakata na kutengeneza magari ya maboksi ya aina mbalimbali. Kuanzia magari madogo, malori ya kawaida, lori la trela, mabasi, kila mtoto akitengeneza kwa kulipambana gari lake kwa nakshi mbalimbali, vile alivyojaaliwa kipaji.

Ndiyo maana nayo pia kuna mengine yalikuwa yanapendeza zaidi machoni kuliko mengine.

Kwenye matairi, watoto wataweka visoda, au kifuniko vya maboksi ya pombe aina ya chibuku.

Maboksi ya yaliyokuwa yakiwekewa pombe ya chibuku, yalikuwa pia yakitumika kutengeneza magari, hasa lori na trela lake.

Hata makopo nayo, yalitumika na watoto kutengeneza magari, ingawa hii kazi yake ilikuwa ngumu zaidi kwani ilibidi kopo likatwe na kunyooshwa na kuungwaungwa kama gereji, huku chini wakiweka mbao na kuifanya kama 'chassis', wakifunga na mipira ya manati kama ndiyo nati.

Matairi ya magari haya yalikuwa ni kandambili iliyokatwa duara na kufanywa tairi.

Magari haya ya makopo yalitengenezwa na watoto 'mafundi' zaidi na wenye uwezo mkubwa na si kila mtoto aliweza kutengeneza.

Watoto wa vijijini, wao hawakuwa na maboksi mengi kutokana na idadi ndogo ya maduka, lakini waliweza kutengeneza magari yao kwa kutumia miti mbalimbali, lakini mara nyingi walitumia matete.

Tena wao walienda mbali zaidi kwani katikati ya matairi, kuna kitu fulani wanafunga, ambacho kinagusana na mti wa chelewa na kutoa mlio au sauti ya gari linalotembea. Wao hawakuwa na magari bubu ambayo hayatoi sauti kama ya watoto wa mjini.

Watoto wa kike walikuwa na kazi ya kutengeneza wanasesere wa vitambaa na udogo, ili hali kila wakati walikuwa wakibuni vitu vya kuchezea.

Ilikuwa ni burudani kuwaona watoto kila mmoja, akiwa na gari lake la maboksi alilolitengeneza mwenyewe akiendesha, haijalishi halitengeza vizuri au vibaya, ili mradi tu linatembea.

Hii ni kwa sababu, wengine walikuwa na vipaji zaidi kuliko wengine. Lakini hii yote iliwafanya watoto wawe wabumifu, kuwa na uwezo wa kutengeneza kitu ambacho wanadhania wanaweza.

Sipati picha watoto wale waliokuwa na uwezo huo, wangekuwa kwenye kizazi cha sasa cha teknolojia, huku viwanda nyingi vikitengenezwa.

Nadhani vitu vingi vya kuchezea watoto, yakiwemo magari na midoli wala isingetoka nje ya nchi.

Ubunifu huu na mwingine mwingi, hasa kuonekana kuwa na uwezo wa kujishughulisha na kazi za mikono, zilifanya vijana wengi wakati ule kuanza kujitegemea mapema, wakiwa na uwezo wa kuondoka nyumbani akiwa na hata miaka 18 na kwenda kuanza maisha wenyewe.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risassi zilimfanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu.

Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini aliyemteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji?

Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina jambo langu-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Sasa kila mmoja alimuona mwenzake vizuri zaidi. Wakatambuana. Wakakumbaniana kwa furaha.

Yaliyofauta hapo ni mazungumzo ya salaam na kukumbushiana yale ya zamani. Ni watu wanaotambuana.

"Nilidhani nitakuja kukuoa Ester, lakini ukahama chuo sikukuona tena."

"Mpenzi, si unajua tena wazazi, walinihamisha kwa nguvu bila kupenda. Kusema kweli nililia sana. Nikakukumbusha sana mpenzi wangu. Leo ni zaidi miaka kumi ndiyo tunaonana kweli Mungu mkubwa."

"Umeoa Jerry?"

"Bado"

"Unasubiri nini?"

"Sijui hata ninachosubiri, ila bado, wewe je?"

Ester alishusha pumzi, kitu ambacho kilimfanya Jerry kujua kuwa itakuwa ni historia ndefu.

Akamtaarifu kuwa amepaki gari mbele, hivyo atamsogeza anapokwenda.

Walikiwa ndani ya gari, Jerry alirudia swali.

"Nilikuuliza, mwenzangu, mpenzi wangu wa zamani wakati tuko chuo, umeolewa?"

"Niliolewa, lakini..."

"Umeachika?"

"Si bora ningeachika, ningeolewa na mwingine. Hata wewe mpenzi wangu wa zamani ningekwambia unioe."

"Sasa."

"Mwenzangu nimeolewa tena kwa ndoa ya Kanisani, na nimezaa mtoto mmoja na mume wangu, lakini amenitelekeza."

"Duh, pole sana mpenzi kwa yaliyokutokea."

"Kwa sasa unaishi wapi?"

"Naishi Ubungo wa mjomba wangu, ila wakati niko na mume wangu, tulikuwa tunaishi Kunduchi."

"Yeye huyo mumeo kwa sasa yupo wapi?"

"Anaishi na huyo mwanamke wake, tena wameoana kwa ndoa ya Kiserikali kwa sababu haruhusiwi tena kuona Kanisani."

"Kwa nini hukuweka pingamizi kwenye ndoa yao?"

"Jerry, yaani mimi hakuniambia chochote, alitoweka tu nyumbani, kumbe alikuwa ameshampangia chumba sehemu, akawa anaishi. Nyumbani kurudi ikawa kwa tabu tabu mwisho, wakaoana bila mimi kujua lolote na baada ya ndoa wakahama na hapo walipokuwa wanakaa. Akawa ndiyo amenitelekeza hivyo na mtoto."




"Na mpaka sasa hujui anapoishi?"

"Nahisihasi tu, lakini nitapajua tu."

"Nimesikitishwa sana Ester. Mimi nilikupenda sana, mimi ningekuoa kusema kweli, lakini wazazi hawakutaka, ukakutana na huyo mtu akakutenda, pole sana."

"Ahsate sana." Alisema Ester na kuonekana maneno ya Jerry yamemuingia na akainamisha kichwa chini, machozi yakaanza kumtoka."

Ikawa kazi ya Jerry kumbembeleza huku akiendesha gari. Ilikuwa ni mara ya pili kwa Jerry kubembeleza wanawake ndani ya wiki moja.

Siku chache zilizopita akiwa na Neema nyumbani kwake Chang'ombe alilazimika kumbembeleza baada ya kumsimulia jinsi alivyoona laivu tukio la mtoto wake kutekwa hadi gari lilipoingia kwenye geti la jumba moja la kifahari eneo la Ubungo Maziwa.

Jerry alilazimika kufanya kazi hiyo kwa sababu tu alimpenda Neema kutoka moyoni, licha ya kwamba tayari alikuwa ameolewa.

Alifanya hivyo ikiwa ni kumuonyesha upendo Neema, pamoja na kwamba anajua kabisa kuwa hatoweza kuwa mpenzi wake wala mkewe.

Na mpaka sasa bado amejivika joho la kumtafuta mtoto, nia ikiwa ni kumsaidia Neema ili arejee kuwa na furaha yeye na familia yake. Furaha ya Neema aliiona ni furaha kwake pia.

Tangu alipomuona Neema kwa mara ya kwanza maeneo ya Makumbusho walipokuwa wananunua matunda, aliingia kwenye moyo wake na hata alipomwita ili amueleze lililo kwenye moyo wake hakutakataa, ila baada ya kumwambia, Neema alimpasha kuwa tayari ameolewa na ana mtoto mmoja.

Hayo yalitokea kabla mtoto hajatekwa.

Leo hii anambembeleza mwanamke mwingine Ester. Mwanamke ambaye walisoma wote chuo mkoani Dodoma, lakini alihamishwa na wazazi wake. Wakati wanasoma, Jerry na Ester walikuwa wapenzi. Uhamisho na kutojua wapi amehamishwa ndiyo sababu ya kutoonana hadi leo hii walipokutana.

Jerry hakujua ajione mwenye bahati au mwenye mikosi. Kuliliwa na wanawake hao.

Gari ilifika maeneo ya Ubungo kituoni. Ester akaomba ashushwe hapo.

"Nilisema nitakufikisha hadi nyumbani kwako, au unamuogopa shemeji?" Jerry alitania.

"Una wazimu wewe, shemeji atoke wapi. Si nilikwambia nakaa na mjomba wangu."

"Kwani kukupeleka hadi kwa mjomba wako nikajitambulishe kuna kosa?"

"Hapana kuna vitu nataka nichukue hapa. Ila Jerry kuna kitu kinanisumbua sana, naomba ushauri wako."

"Kitu gani hicho mpenzi?"

"Basi tu. Mimi sitaki kumwambia hapa. Ni hadithi ndefu sana na hapa tutachelewa. Leo si Jumapili? Kama utakuwa na muda Jumanne njoo hapa hapa, nikuchukue nikupeleke nyumbani. Nyumbani kwa mjomba wangu. Hakuna tatizo wala usiogope, mimi ni mkubwa, nimeshaolewa nimezaa, kuna nani tena anaweza kunichunga?" Bado Ester alikuwa akiongeza na Jerry akiwa ndani ya gari, lakini nikiwa limesimama akiwa anajiandaa kuteremka.

"Jambo lenyewe ni hili la jamaa aliyekutelekeza au kuna jingine jipya?"

"Usiwe na haraka Jerry, tutaongea vizuri, halafu wewe najua utanishauri vizuri ili limalizike, maana limenichosha. Limenikinahi kweli mpenzi."

"Sawa, mimi nimekuelewa, nimeamua kukusaidia kwa hilo, kama ni ushauri mimi niko tayari. Nitakuja hapa Jumanne."

"Nitashukuru sana." Ester aliteremka kwa madaha ndani ya gari. Kabla hajafunga mlango alimbusu Jerry shavuni huku baadhi ya watu waliokuwa pembeni ya barabara wakiwa mashuhuda.

"Ahsante uwe ya siku njema." Jerry alijibu baada ya kupigwa busu mwanana.

Akiwa anarejea nyumbani baada ya kuachana na mwanamke huyo, Jerry alikuwa na mawazo tele kichwani.

Aliona kabisa kuwa nafasi yake kwa Ester bado ipo.

Aliona dalili zote kuwa Ester anahitaji warudiane. Tatizo ni kwamba tayari alikuwa ameshalihamisha penzi kutoka kwake baada ya kuachana miaka mingi.

Penzi lake kwa sasa limetua kwa Neema. Neema ambaye ni mke wa ntu. Neema ambaye anajua kabisa kuwa hawezi si tu kuwa mke wake, lakini hata kuwa mpenzi wake.

Siku zote penzi ni kizungumkuti. Penzi ni kitu cha ajabu sana. Anayekupenda wewe haumpendi. Unayempenda ana mwingine. Hakujua afanyeje.

Faraja yake pekee aliyoipata ni wanawake wao wote wawili, kulia mbele yake. Kila moja alimuona wa thamani kwake.

Kila mmoja akitaka msaada kutoka kwake. Hakujua mwisho wa yote nini kitatokea.

Itaendelea Jumapili

hapo walipokuwa wanakaa. Akawa ndiyo amenitelekeza hivyo na mtoto."

INAENDELEA JUMAPILI



# MWIJAKU AKUBALIANA WANAWAKE KUTUNZWA

MWIGIZAJI na mtangazaji, Mwijaku, ameingilia mjadala unaoendelea wa uhalali wa wanawake kupewa pesa, akisema wana haki ya kutunzwa kutokana na vitabu vya Mungu vimetoa haki hiyo.

'Vitabu vya Mungu vinasema mwanamke atazaa kwa uchungu na Mwanamume utatafuta kwa jasho, hivyo ni hekima sana, mwanamke ana haki ya kupewa kwani mwanaume ni kiongozi wa familia" amesema.

Ameongeza kuwa mwanamke akitoa pesa kwenye familia itakuwa ni mapenzi yake na sio kumpangia.



# LULU, WEMA WAZIDI KUCHEFUANA

MWIGIZAJI nyota wa Bongo Muvi, Elizabeth Michael, maarufu kama Lulu, ameingia katika bifu kali na msanii mwenzake Wema Sepetu, baada ya kutajwa kuwa chanzo cha kifo cha Steven Kanumba.

Wema alimtaja Lulu, wakati akimuoji mama Kanumba katika kipindi chake cha mapishi, jambo ambalo lilimkera mrembo huyo na kuita kitendo hicho cha kinafiki.

"Sipendi unafiki, Sikufurahishwa na alichofanya wakati anamuhoji mama Kanumba, niliamua kumuondoa katika ukurasa wangu wa Istagram kwa kweli, kama yeye anahisi amenikosea basi atanitafuta," amesema.

# Hamisa usemayo yanatoka moyoni?

MWANAMUZIKI na mwanamitindo maarufu nchini, Hamisa Mobetto, ameibua mjadala mkali baada ya kueleza ugonjwa wa corona unapeperusha ndoa yake.

Mrembo huyo kupitia 'Insta Story' aliandika hana bahati ya kuolewa kutokana na ugonjwa huo kuja wakati yupo katika mipango ya harusi yake.

"Yani kila nikitaka kuolewa corona hiyoo, sijui kwa nini?" ameandika Hamisa na kuwafanya baadhi ya wafuasi wake kumtupia lawama kuwa anausingizia ugonjwa huo tu, wakati mwenyewe hana mpango wa kuolewa.



## HABARI MICHEZO




# ARTETA:

## MAWAZO YALIMSUMBUA AUBAMEYANG

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta, amekubali nahodha wa timu hiyo, Pierre-Emerick Aubameyang alikuwa na msongo wa mawazo, baada ya mama yake kuwa mgonjwa.

Aubameyang alirejea kikosini katika kichapo cha katikati ya wiki dhidi ya Wolves, akiwa amefanya mazoezi peke yake na alikosa mechi tatu kwa sababu ya matatizo ya kifamilia.

Arteta alitarajiwa kuwa tayari kurejea kikosini katika safari ya mchezo wa jana Jumamosi dhidi ya Aston Villa, licha ya kuelemewa na mzigo mzito wa mawazo katika wiki za hivi karibuni.

Arsenal kwa sasa ipo katika nafasi ya 10 ikiwa na alama 31 baada ya kucheza michezo 22 ya Ligi Kuu England msimu huu.

# PIQUE AELEZEA PENZI LAKE KWA SHAKIRA




**BARCELONA, Hispania**

NYOTA wa Barcelona, Gerard Piqué ambaye ana umri wa miaka 34 ameelezea jinsi alivyokutana na mkewe, Shakira Isabel Mebarak Ripoll (44)..

"Mara yangu ya kwanza kukutana na Shakira nilikuwa Madrid wakati tulikuwa tukifanya video ya 'Waka Waka' kabla ya fainali za Kombe la Dunia la 2010 na hapo ndipo niliomba namba yake," alisema Pique.

"Baadaye Shakira alikwenda Afrika Kusini kabla yetu (kikosi cha Timu ya Taifa ya Hispania) wakati alikuwa akiimba kwenye sherehe ya ufunguzi wa michuano ya Kombe la Dunia. Nilimtumia ujumbe kwenye simu na kumuuliza hali ya hewa ilikuwaje kwa sababu tulikuwa tunatarajia kufika huko katika siku chache zinazofuata.

"Hili ni swali la kawaida la kijinga unaloandika na kawaida hupata jibu kama 'Ni baridi, njoo na koti'. Lakini haikuwa hivyo aliandika ujumbe marefu, akielezea mabadiliko ya hali ya hewa jinsi kulivyo na joto siku nzima.

"Nilifikiria nikasema, hii sio kawaida'. Ilikuwa katika maelezo yake hayo ambapo niliweza kusema kulikuwa na kupendana kati yetu. Tulianza kutumiana ujumbe wakati wote wa mashindano ya Kombe la Dunia.

"Lakini, nafasi pekee ambayo nilikuwa nayo ya kumwona ilikuwa kama tungefika hatua ya fainali, kwani wakati huo alikuwa na ratiba ya kutumbuiza kwenye sherehe ya kufunga fainali za dunia. Nilimwambia kwamba kama njia ya kumwona ni hadi siku ya fainali, basi nitafanya hivyo.

"Mungu ni mwema tukafika hadi fainali, ilikuwa jambo nzuri zaidi ambalo nilikuwa nimelipata tangu Hispania tushinde Kombe la Dunia na hakika nikafanikiwa kukutana na mpenzi wa maisha yangu. Niliondoka Afrika Kusini nikiwa mtu mwingine kabisa. " aliongeza Gerard Pique.

# Tuchel anataka mabeki watatu Chelsea

**LONDON, England**


INAAMINIKA kwamba nyota wa kikosi cha RB Leipzig, Dayot Upamecano ni miongoni mwa orodha ya majina yaliyopo kwenye mpango wa Kocha Mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel.

Ripoti zinaeleza kuwa Tuchel ambaye ni mrithi wa mikoba ya, Frank Lampard macho yake kwa upande wa usajili yanatazama nyota ambao wanashiriki Ligi Kuu Ujerumani, maarufu Bundesliga na anahitaji beki wa kati.

Tuchel tayari ameanza kazi ndani ya Stamford Bridge huku akionekana kuleta mabadiliko ndani ya timu na ana matumaini ya kuboresha zaidi kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao.

Kwa mujibu wa gazeti la Bild, Tuchel katika akili yake kuna majina ya mabeki watatu ambao ni Niklas Sule na David Alaba wa Bayern Munich pamoja na Upamecano.

Alaba mwenye umri wa miaka 28 pia anatajwa kuwaniwa na Liverpool pamoja na Real Madrid.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO: NINAELEKEA MWISHO KATIKA SOKA

Nyota huyo afunguka amecheza kwa kiwango bora kwa muda wa miaka 20, na atafanya hivyo kwa...

**TURIN, ITALIA**

CRISTIANO Ronaldo anajua kabisa kwamba, hawezi kucheza soka kwa miaka mingine 20, lakini ameahidi kucheza kwa kiwango cha asilimia kwa muda uliosalia katika maisha yake ya soka, wakati akiwa ametimiza umri wa miaka 36, juzi Ijumaa.

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or, katika miaka 20 ya soka la kulipwa bado ana kiwango thabiti na tayari amefunga magoli 22 na kutoa pasi za mwisho 23 katika mshindano yote akiwa na Juventus msimu huu.

Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno katika siku yake ya kuzaliwa aliweka posti katika akaunti yake ya Instagram, aliandika: "Miaka 36, haiaminiki! Nahisi kama imeanza jana, lakini safari hii tayari ina hadithi na matukio lukuki ya kukumbukwa. Mpira wangu wa kwanza, timu yangu ya kwanza, bao langu la kwanza... muda unakimbia.

"Kutoka Madeira mpaka Lisbon, Lisbon hadi Manchester, Manchester hadi Madrid, Madrid hadi Turin, lakini juu ya yote kutoka kwenye moyo wangu. nimetoa kila kitu ambacho nilipaswa kutoa, siwezi kurudi nyuma na kila wakati ninajaribu kutoa kilicho bora kadri ya uwezo wangu.

"Ikiwa nina sherehekea miaka 36 ya kuzaliwa na miaka 20 ya kazi yangu, nasikitika kusema siwezi kuahidi kucheza kwa miaka 20 mingine, lakini naweza kuahidi ilihali naendelea kusonga basi hutopokea si pungufu ya 100% kutoka kwangu.

"Asanteni kwa mara nyingine kwa sapoti yenu na ujumbe wenu nzuri katika siku ya leo, hii inamaana kubwa kwangu wote mna nafasi maalumu katika moyo wangu."

## KWA UFUPI

**CITY YAMFIKIRIA HAALAND**
MANCHESTER City wanaamini kwa kushinda taji la Ligi Kuu England msimu huu kutawahakikisha nafasi ya kuwapiku Chelsea kumsajili straika wa Borussia Dormund, Erling Braut, Haaland ambaye ana umri wa miaka 20. **(Star)**

**POGBA, UNITED KITAELEWEKA**
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amebainisha kiungo wa Ufaransa, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 27, anaweza kumsaini mkataba mpya pale Old Trafford. **(Guardian)**

**SALAH KUMKIMBIA MBAPPE**
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah (28), anaweza kuwa mchezaji wa kwanza kuondoka kama Liverpool watakaribia kumsajili straika wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe ambaye ana umri wa miaka 22, kipindi hiki cha majira ya joto. **(Marca)**

**ALABA ANUKIA CHELSEA**
CHELSEA itajaribu kuwapiku Real Madrid kumsajili mlinzi wa kati wa Bayern Munich na Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, ambaye anapanga kuondoka kwa mabingwa wa Ujerumani baada ya mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu. **(Guardian)**

**CHELSEA KUSAKA MABEKI**
CHELSEA ina matumaini kuwasajili walinzi wawili, Dayot Upamecano wa Leipzig mwenye umri wa miaka 22, na nyota wa Bayern Munich, Niklas Sule ambaye ana umri wa miaka 25. **(Goal)**

**LINGARD ATAJWA WEST**
WEST Ham haina haraka ya kufanya uamuzi kuhusu kumsajili kwa mkataba wa kudumu kiungo wa Timu ya Taifa ya England na Manchester United, Jesse Lingard ambaye ana umri wa miaka 28. **(Standard)**

**LEICESTER YAINGIA SOKONI**
LEICESTER City ipo kwenye mazungumzo na kiungo wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 23, kuhusu mkataba mpya utakaomfanya alipwe mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki. **(Mail)**

**ODEGAARD ANOGEWA ARSENAL**
KIUNGO wa Norway, Martin Odegaard, mwenye umri wa miaka 22, anaweza kusaini mkataba wa kudumu na Arsenal kama Zinedine Zidane atabakia kuwa Kocha wa Real Madrid. **(Eurosport)**

**OVERMARS KUREJEA EPL**
WINGA wa zamani wa Arsenal, Marc Overmars anataka kurudi klabuni hapo kama Mkurugenzi wa Soka. Kwa sasa anafanya kazi kama hiyo kwenye kikosi cha Ajax ya Uholanzi. **(De Telegraaf)**

**MAQUIRE AITULIZA UNITED**
MANCHSTER United haina tena mpango wa kusajili mlinzi wa kati mpya kwa sababu kiwango cha beki wao, Harry Maguire ni cha kuvutia. **(Manchester Evening News)**

**CHELSEA KUMSAJILI HAZARD**
CHELSEA inampango wa kumsajili tena fowadi wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Eden Hazard ambaye ana umri wa miaka 30, kutoka Real Madrid ifikapo kipindi cha majira ya joto. **(Defensa Central)**



## HABARI MICHEZO

# MANGUNGU AAHIDI SIMBA ITAPATA MAFANIKIO AFRIKA

**Na Saada Akida**

MGOMBEA wa nafasi ya uenyekiti katika klabu ya Simba, Murtaza Mangungu amesema kilichomsukuma kuwania nafasi hiyo ni kutaka kutimiza ndoto ya kuipa mafanikio ya juu zaidi klabu hiyo.

Mangungu na Katibu Mwenezi wa zamani wa Simba, Juma Nkamia wanatarajia kuchuana katika uchaguzi mdogo wa klabu hiyo utakaofanyika leo kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.

Uchaguzi huo ni wa kujaza nafasi iliyoachwa na Swedi Mkwabi ambaye alitangaza kujiuzulu hapo mwaka juzi.

Mgombea huyo alisema endapo atachaguliwa katika nafasi hiyo, atalifanyia kazi suala la mgongano lililopo katika ya Simba na Tume ya Ushindani Nchini (FCC), na hatimaye kumaliza sintofahamu iliyopo.

Alisema anaamini FCC itatoa mwongozo na misingi mizuri ili kuiona Simba inafikia malengo yake. "Ninataka kwenda kushirikiana na wanachama wenzangu, yale mambo mazuri ambayo yamefanyika tangu awali tuweze kuyaongezea nguvu," alisema Mangungu.

Kuhusu suala la Mangungu, kupandikizwa na mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed Dewji (Mo), alisema hana hakika na hilo na kamwe hawezi kupandikizwa na mtu yoyote kwa sababu yeye ni mtu anayejiamini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchanguzi, Boniface Lihamwike alisema baada ya kupita hatua mbalimbali sasa mchakato wa uchaguzi huo umekamilika na leo siku maalum na muhimu kwa wanachama wa Simba kutafuta kiongozi atakayewafaa.

Lihamwike alisema uchaguzi huo utahusisha wagombea wawili ambao ni Nkamia na Mangungu baada ya wengine kuenguliwa na baadhi kuamua kujitoa kwa sababu zao mbalimbali.

"Uchanguzi utakuwa ni sehemu ya ajenda ya mkutano mkuu, wagombea waliopo ni Nkamia na Mangungu, wanatakiwa kufuata maelekezo na sheria za uchaguzi ikiwamo kutoruhusiwa kufanya kampeni au kubeba chochote, iwe kinaashiria kupiga kampeni ndani ya ukumbi huo,"alisema Lihamwike.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema wanachama wanatakiwa kutumia fursa hiyo vizuri kwa kumpata mwenyekiti ambaye ataingia kwenye Bodi ya Wakurugezi wa klabu hiyo iliyoko chini ya Mo.

"Kesho (leo), tiketi zitauzwa ukumbini kwa ajili ya kuwasaidia wanaotaka kwenda uwanjani wasipate shida kuhusu kutoka na kuhangaika na mambo ya tiketi za kwenda kuangalia timu yao," alisema Manara.

Aliongeza katika mkutano wa leo wanatarajia kutangaza zawadi maalum ambayo itakuwa 'suprise' kwa ajili wanachama lakini akiweka wazi itahusiana na timu yao ya Simba Queens, ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.




Mwenyekiti Kamati ya Uchaguzi ya Klabu ya Simba, Boniface Lihamwike (kulia), akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na maandalizi ya uchaguzi mdogo wa klabu hiyo unaotarajiwa kufanyika leo jijini Dar es Salaam. Kushoto ni mjumbe wa kamati hiyo, Gerald Mongella.**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waamuzi Zanzibar wailiza Uhamiaji

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Uhamiaji imetupa lawama kwa waamuzi wanaochezesha Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kwa kusema wanashindwa kutafsiri vyema sheria 17 za soka.

Uhamiaji wametoa kauli hiyo baada ya kufungwa bao 1-0 na Kilimani City katika mchezo wa ligi hiyo uliochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Uhamiaji, Mutala Ahmed alidai timu yake ilipoteza mchezo huo kwa sababu waamuzi walionekana kuwabeba wapinzani wao na kuacha kufuata sheria za soka.

Ahmed alisema waamuzi waliochezesha mchezo huo waliziacha faulo za wazi ambazo walistahili kupata na hivyo kuwanyima nafasi ya kupata mabao na kupunguza mashambulizi.

"Waamuzi walikuja na matokeo yao mkononi kwa kuwapa ushindi wapinzani wetu. Waamuzi bado ni tatizo katika Ligi za Zanzibar, wanaamua wanavyotaka wao na si sheria za soka zinavyotaka, hii inatuumiza kama timu pamoja na kutuvunja moyo," alisema Ahmed.

Kuhusu kikosi chake katika mchezo huo alisema wachezaji walicheza vizuri na walistahili kupata ushindi licha ya mechi hiyo kuwa na ushindani katika dakika zote 90.

Aliongeza licha ya kupoteza mchezo huo, bado hawajakata tamaa ya kutimiza ndoto zao wa kupambana na hatimaye kucheza Ligi Kuu Zanzibar katika msimu ujao.

# Polisi Tanzania kamili Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA chaguo la kwanza wa Polisi Tanzania, Mohamed Yusuph ameanza mazoezi ya pamoja na wachezaji wenzake kwa lengo la kurejea dimbani kuitumikia timu hiyo katika mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara, imeelezwa.

Kipa huyo tegemeo alikuwa majeruhi na kusababishwa kucheza mechi chache za mzunguko wa kwanza kama ilivyotarajiwa na klabu yake.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Polisi Tanzania, Frank Lukwaro aliliambia gazeti hili mabosi wa timu hiyo wamefurahi kuona mlinda mlango huyo amerejea na wanaimani ataongeza nguvu katika kikosi chao.

"Golikipa wetu namba moja ameanza mazoezi na wenzake, utakumbuka aliumia mwanzoni tu mwa ligi na muda wote huu alikuwa kwenye matitabu, tunashukuru ameshapona, na hivi karibuni ataonekana uwanjani," alisema Lukwaro.

Alisema tayari kikosi hicho kimeingia kambini kujiandaa na mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao unatarajiwa kuwa mgumu zaidi kwa sababu kila timu inahitaji kuchukua pointi tatu katika kila mechi na kufikia malengo yake.

"Timu imeingia kambini na inafanya mazoezi kila siku jioni kwenye Chuo cha Wanyamapori Mwika, lengo ni vijana wawe imara na tayari kupambana kumalizika msimu, tunajua tunakwenda katika kipindi chenye ushindani, tumejipanga kwa hilo," alisema Lukwaro.

Yusuph anarejea, wakati timu hiyo ilikuwa ikimtumia Msafiri Mkumbo kama kipa namba moja huku Peter Manyika akiwa ni mlinda mlango wa akiba.

Hata hivyo, kipa huyo anapishana na Manyika ambaye ameondoka kwenye klabu hiyo katika kipindi cha dirisha dogo la usajili, ambapo amejiunga na Dodoma Jiji FC ya jijini Dodoma.

Polisi Tanzania inayotumia Uwanja wa Ushirika Moshi mkoani Kilimanjaro kama uwanja wake wa nyumbani ipo kwenye nafasi ya saba, ikiwa na pointi 23 baada ya kucheza michezo 18.

Kikosi cha Polisi Tanzania kitashuka tena dimbani kuwania taji la Ligi Kuu Bara ifikapo Februari 23, mwaka huu ugenini dhidi ya Gwambina FC kwenye Uwanja wa Gwambina ulioko Misungwi jijini Mwanza.

Simba ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 wakati Yanga yenye pointi 44 inaongoza katika msimamo na Ihefu FC ya jijini Mbeya yenye pointi 13, inaburuza mkia.

# Michezo

Jumapili Februari 7, 2021

Nipashe




## Ronaldo: Ninaelekea mwisho katika soka

HABARI UK 22

# Ubingwa Yanga SC utapatikana namna hii

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kusota kwa misimu mitatu mfululizo, Yanga inaonekana imedhamiria kurejesha heshima yake kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2020/21.

Awali, wakati Ligi Kuu Tanzania Bara inaanza viongozi wa klabu hiyo walibuni kauli mbiu yao 'tuna jambo letu msimu huu', ambao umeendelea kutumika si kwa viongozi tu, bali wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kongwe hapa nchini.

Mkurugenzi wa Uendeshahi wa Kampuni ya GSM ambao ni wadhamini wa Yanga, Hersi Said ameonekana tangu mwanzo akifanya kazi kubwa, hasa ya kuwaunganisha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kushirikiana kwa lengo la kurejesha furaha waliyoizoea.

Hersi ametamba wamejipanga kupambana kuhakikisha wanatwaa ubingwa kwa kufanya usajili mzuri ambao umeimarisha kikosi chao.

"Tunasema ubingwa ni wetu si kwa maneno matupu, malengo yetu yanatokana na usajili wa nguvu tulioufanya ambao umewashangaza si wapinzani wa klabu ya Yanga tu, bali hata wanachama na mashabiki wa klabu hiyo," alisema Hersi.

Katika kuimarisha kikosi cha Yanga, klabu hiyo ilisajili wachezaji nyota watatu kutoka AS Vita ya Jamhuri ya Kidemorasia ya Congo (DRC), Mukoko Tonombe na Tuisila Kisinda, Waghana Michael Sarpong, Yacouba Songne, na Carlos Carlinhos kutoka Angola.

Pia hapa nchini Yanga iliongeza nguvu kwa kuingia mkataba na Bakari Mwamnyeto kutoka Coastal Union, Yassin Mustapha aliyekuwa Polisi Tanzania na nyota wa Mtibwa Sugar, Kibwana Shomari na dirisha dogo iliwaleta Saido Ntibazonkiza, Dickson Job na Fiston Abdulrazack.

Wachezaji wao hawakuwaangusha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo, kwani wamecheza mechi 18 za Ligi Kuu Tanzania Bara bila kupoteza mechi yoyote ile.

Yanga inaongoza ligi ikiwa na pointi 44, baada ya kushinda mechi 13 na sare michezo mitano iliwafunga Azam bao 1-0 na kuchukua pointi tatu lakini ikawabana watani zao Simba kwa sare ya bao 1-1.



Beki wa Tottenham Hotspur, Eric Dier (kushoto), akimfanyia faulo mchezaji wa Chelsea, Timo Werner, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja Tottenham Hotspur juzi usiku. Chelsea ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, AZAM FC HATUMWI MTOTO

## Ni mechi nyingine ya 'kiporo' ambayo itatoa 'picha' kuelekea katika mbio za...

**Na Saada Akida**

NENO pointi tatu ndio linalozunguka kichwani kwa Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi, Simba, Didier Gomes, kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kuanzia saa 10:00 jioni leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Hicho ni kiporo cha pili cha Simba, mabingwa watetezi baada ya Alhamisi kuikabili Dodoma FC na kupata ushindi wa mabao 2-1 na kuendelea na mbio zake za kutetea taji hilo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gomes alisema anatambua mchezo huo utakuwa na ushindani kwa sababu kila timu inahitaji pointi tatu ili kujiweka katika nafasi bora ya kutimiza malengo yake.

Gomes alisema amewaandaa wachezaji wake kupambana na kucheza katika kiwango cha juu kutokana na kuwafahamu wapinzani wao pia wanahitaji ushindi ili kurejea kwenye vita ya kuwania ubingwa wa msimu huu.

Mfaransa huyo alisema ushindi walioupata dhidi ya Dodoma jiji FC ulikuwa ni mwanzo mzuri kuelekea mechi ya leo na vile vile kujiandaa na mechi za hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Mechi itakuwa ngumu, lakini nimeongea na wachezaji wangu ambao wameniambia wataingia uwanjani kwa kazi moja ya kupambana ili kupata pointi tatu muhimu, ushindi utatusaidia kupunguza tofauti ya pointi ambazo tumeachwa na anayeongoza ligi (Yanga),".

"Tuna kazi kubwa ya kufanya, Azam FC wamejiandaa na pia wanahitaji pointi tatu, tunaenda uwanjani kwa kuwaheshimu wapinzani na wachezaji wanatambua nini wanaenda kufanya," alisema Gomes.

Alisema kikosi chake kipo fiti hakuna mchezaji ambaye ni majeruhi na kuwataja nyota Joash Onyango na John Bocco, nayo afya zao zimeimarika.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alisema baada ya mechi hiyo kikosi chao kitabakia kambini na wanatarajia kuondoka nchini na kuelekea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), keshokutwa Jumanne.

Manara alisema wameamua kuondoka nchini mapema ili kupata muda wa kujiandaa zaidi na mchezo wao wa hatua ya makundi dhidi ya AS Vita utakaochezwa Februari 13, mwaka huu mjini Kinshasa.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Mrundi Vivier Bahati, alisema kikosi chao kipo kamili na wataingia uwanjani wakiwaheshimu wapinzani wao.

Bahati alisema wamejiandaa kucheza soka la kushambulia na kuzuia huku wakiwanyima Simba nafasi ya kucheza mpira kama ilivyozoeleka.

"Simba ni timu nzuri, ukizingatia wanacheza mechi za kimataifa hivyo tutaingia kwa kuwaheshimu, tumeona upungufu wao na kufanyia kazi ikiwamo kutowaruhusu wasicheze mpira, ukifanya hivyo tuna imani tutakuwa tumewashika," alisema kocha huyo.

Katika msimamo wa ligi, Simba yenye pointi 38 iko nyuma ya vinara Yanga ambao wamejikusanyia pointi 44, wakicheza mechi mbili zaidi huku Azam FC yenye pointi 32 wakiwa kwenye nafasi ya tatu.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042